# Nipashe

Jumamosi Aprili 3, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580539

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

**Askofu** akemea ubinafsi, usaliti, uroho madaraka



UKURASA 3

**Mwenyekiti** wa mtaa auawa kwa kuchomwa kitu chenye ncha kali

UKURASA 4



# Shoo: Samia amekuja kuleta habari njema

• **Maaskofu** wataka Watanzania wamwombee, wahimiza kumuenzi JPM kwa mema aliyoyafanya... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**KASI YA RAIS SAMIA YAMWIBUA MBUNGE**

KASI ya Rais Samia Suluhu Hassan imemwibua Mbunge...

UKURASA WA 5

**WACHIMBAJI WADOGO HATARINI KUKOSA AJIRA**

IDADI kubwa ya wachimbaji wadogo wa dhahabu katika...


## Sakata mahindi latua kwa wakuu wa nchi

UKURASA 5



Kijana James Erick Mbogo akiwambwa msalabani wakati wa igizo la mateso ya Yesu Kristo, katika ibada ya Ijumaa Kuu kwenye Kanisa Katoliki Parokia ya Bikra Maria Consolata Mshindo, mjini Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




# Kilio vifurushi, gharama za simu chatawala kila kona

UK. 3

**MICHEZO** **SIMBA, AS VITA HATUMWI MTOTO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Waumini wa Kanisa la Angalikan Dayosisi ya Central Tanganyika wakisalimiana na wachungaji wa kanisa hilo, baada ya kumalizika kwa ibada ya Ijumaa Kuu iliyofanyika jana. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# Maaskofu wataka Watanzania kumuenzi JPM

**Na Mwandishi Wetu**

MAASKOFU wa makanisa mbalimbali nchini, wamewataka Watanzania kumuenzi aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, kutokana na mambo mema aliyoifanyia nchi wakati wa uongozi wake.

Rai hiyo waliitoa jana wakati wa ibada za Ijumaa Kuu zilizofanyika sehemu mbalimbali ikiwa kukumbuka kuteswa hadi kufa kwa Mwokozi wao Yesu Kristo yapata miaka 2,000 iliyopita. Kitaifa, ibada ya Ijumaa Kuu ilifanyika katika Kanisa la Umoja wa Makanisa ya Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Akihubiri katika ibada hiyo, Makamu Mwenyekiti wa CCM, Askofu Alex Malasusa, alisema Watanzania wana jambo la kujifunza kupitia uongozi wa Hayati Dk. Magufuli kwa sababu uongozi wake ulikuwa wa kipekee.

Malasusa ambaye ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP), alisema Magufuli amefanya mambo makubwa ndani ya miaka michache ambayo huenda yangefanywa kwa miaka mingi.

"Katika maisha ya uhai tunayopewa na Mungu binafsi kupitia Hayati Magufuli, natamani sote tujifunze kwamba si wingi wa miaka tunayoishi duniani ndiyo inayokumbukwa au siyo wingi wa miaka ya utumishi unayoifanya ili watu wamkumbuke bali siku zote tujiulize umefanya nini katika kusudi la Mungu katika kipindi ulichopewa katika nafasi yako," alisema Malasusa.

Akitoa salamu za CCT, Dk. Malasusa alisema jumuiya hiyo ina imani kubwa na Rais Samia na wanampongeza kwa kupokea kazi hiyo na kuwapongeza Watanzania kwa utulivu kwa sababu mahali pengine duniani huwa haitokei hivyo.

Pia aliwataka Watanzania kuendelea kumwomba Mungu, kuchukua tahadhari ili kuepuka madhara ya ugonjwa wa virusi vya corona.

**MASANGWA ANENA**

Naye Askofu wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini Kati (Arusha), alisema Hayati Magufuli wakati wa uongozi wake alijitoa kulitumikia taifa na kuna mambo mengi ameyafanya ambayo yatabaki kuwa alama ya kukumbukwa.

"Tumeona Hayati Rais John Magufuli, alivyojitoa kwa hali na mali. Nakumbuka alisema amejitoa sadaka kwa ajili ya Watanzania maskini, hivyo kila mwananchi amwombee kwani alijitoa kama Yesu Kristo kwa ajili ya taifa letu," alisema.

**ASKOFU CHEYO**

Naye Askofu Mkuu wa Kanisa la Moravian Tanzania, Dk. Alinikisa Cheyo, alisema msiba wa Rais Magufuli umeudhihirishia ulimwengu kuwa Tanzania ni nchi yenye amani na utulivu kuliko mataifa mengine duniani kutokana na kuomboleza bila kubaguana kwa misingi ya dini, makabila wala itikadi za kisiasa.

Aliyasema hayo wakati wa Ibaada ya Ijumaa Kuu ambayo ilifanyika katika Kanisa la Moravian Tanzania, Ushirika wa Iwambi jijini Mbeya.

Askofu Cheyo ambaye ni Mwenyekiti wa CCT, alisema ushirikiano na umoja unaoendelea kuonyeshwa wakati huu maombolezo unayafanya baadhi ya mataifa duniani kuona wivu, hivyo akawataka wananchi kuendelea kushikamana.

Alisema ibada ya mazishi ya Hayati Dk. Magufuli iliendeshwa na Kanisa Katoliki lakini walialikwa na viongozi wa madhehebu mengine wakiwamo Waislamu hali ambayo alisema inadhihirisha upendo wa hali ya juu miongoni mwa Watanzania.

"Tunatakiwa kuuendeleza upendo huu maana siyo mataifa mengi yanapenda, tumeonyesha kupendana kwa kiwango cha juu sana. Tuliacha tofauti zetu zote na kwa mara ya kwanza niliona Mufti wa Tanzania (Sheikh Abubakar Zubery) amekaa katikati ya maaskofu," alisema.

**ASKOFU KONKI**

Mkoani Manyara, Askofu Mkuu wa Kanisa la Elimu Pentekoste Tanzania, Peter Konki, amewahakikisha Watanzania kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ni kiongozi makini, hivyo wamuamini kuwa miradi yote ataiendeleza iliyokuwa ikitekelezwa na hayati Rais John Magufuli.

Alisema Rais Samia ni kiongozi makini hivyo Watanzania wasiwe na hofu, kwa kuwa nchi iko salama.

"Makamu wa Rais Philip Mpango na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa wakikaa na mama (Rais Samia), watafanya taifa kuwa salama sana," alisema Konki.

Aliongeza: "Kuna sauti juzi nikiwa madhabahuni ilinijia, inasema hivi hamuwezi kumshukru Mungu, kwa kazi aliyoifanya Magufuli, mnabaki kunung'unika?" Alihoji na kuongeza, tangu siku hiyo niliacha kunung'unika nikaanza kuomba na kumshukuru Mungu na sasa nimeanza kusahau msiba".

Pamoja na mambo mengine, Askofu Konki, ameishauri serikali isikubali wachochezi walioikimbilia nje ya nchi, wakaendelea kuichafua nchi.

**ASKOFU MWENDA**

Askofu wa KKKT Dayosisi ya Ruvuma, Amoni Mwenda, aliwakumbusha Watanzania kuona umuhimu wa kutulia nyumbani wakati huu wa maombolezo badala ya kwenda kufanya mambo mitaani yasiyo mpendeza Mungu.

Alisema hayo wakati wa Ibada ya Ijumaa Kuu kwenye ibada iliyofanyika kwenye Kanisa Kuu la KKKT Usharika wa Songea.

Alisema wakati huu wa maombolezo na Sikukuu ya Pasaka wananchi watumie kumwomba Mungu na kuyakumbuka mema aliyoyafanya Hayati Magufuli wakati wa uhai wake kwa kujenga miundombinu ya barabara, zahanati, vituo vya afya na hospitali, pamoja na huduma ya umeme.

Kadhalika, aliwaomba Watanzania kuona umuhimu wa kudumisha amani katika kipindi chote cha Sikukuu ya Pasaka, huku wakiendelea kumwombea Hayati Dk. Magufuli.

●**Imeandikwa na Romana Mallya (Dar), Allan Isaack (Arusha) Jaliwason Jasson (Babati), Gideon Mwakanosya (Songea) na Nebart Msokwa (Mbeya).**

# Shoo: Samia ameleta habari njema

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fedrick Shoo, amesema ana imani kwamba Mungu atamtumia Rais Samia Suluhu Hassan, kuleta habari mpya ya matumaini kwa Watanzania wote.

Vilevile amewataka wale Watanzania wenye fikra zilizojengeka katika mfumo dume kwamba wanawake hawawezi kwenye uongozi, wakumbushwe habari za kinamama waliotumiwa na Mungu, siku ya kufufuka kwa Yesu Kristo.

Alisema Watanzania wengi, wana matumaini makubwa na Rais Samia na kuwataka waumini wa kanisa hilo kumwombea ili Mungu amjalie awe mjumbe wa kuleta habari njema za matumaini mapya kwa taifa.

Dk. Shoo ambaye ni Askofu wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini, alikuwa akitoa salamu za Sikukuu ya Pasaka za kanisa hilo jana kabla ya ibada ya Ijumaa Kuu iliyofanyika katika Kanisa Kuu la KKKT Moshi Mjini.

"Tunapaswa kumshukuru Mungu kwa kutupa Rais ambaye ameitwa mbele ya haki (Hayati Dk. John Magufuli). Kwa ajili hiyo, nitumie fursa hii kwa mara nyingine kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kupokea kijiti cha uongozi wa nchi yetu na kuwa rais wa sita," alisema na kuongeza:

"Binafsi ninamwombea na ninawasihi Watanzania wenzangu wote kuendelea kumwombea ili Mungu amjalie Rais wetu afya njema, ujasiri, roho ya upendo, hekima na busara ili aweze kuliongoza vyema taifa hili ambalo Mungu ametupa nchi yetu Tanzania."

"Kama Mungu alivyowatumia wale kinamama siku ya kufufuka Yesu Kristo, nina imani kabisa kama vile kina mama walivyokuwa wa kwanza kushuhudia tukio la kufufuka Yesu Kristo na wakawa wa kwanza kupeleka habari njema za matumaini mapya kwa wale wanafunzi.

"Ndivyo hivyo ninavyoamini ya kwamba Mungu atamtumia Rais wetu (Samia), ambaye katika historia ndiye mwanamke wa kwanza kuwa Rais wa nchi hii kwamba ataleta habari mpya ya matumaini kwa Watanzania wote," alisisitiza.

Aidha, Dk. Shoo katika salamu zake alisema anaimani kwamba kwa Rais Samia, Mungu ameweka jambo ndani yake siyo leo wala jana, lakini tangu utoto wake kwamba siku moja atamwinua na kumfanya kuwa Rais wa Tanzania.

**ASKOFU MASSANGWA**

Mkoani Arusha, Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini Kati ya KKKT, Dk. Solomon Massangwa, alisema kanisa linatarajia kuwa na Rais Samia na wasaidizi wake, wataijenga nchi na kuiweka katika mpangilio unaotakiwa.

Pia alisema Rais Samia na viongozi walio chini yake, wataondoa baadhi ya vikwazo vilivyokuwa vinasababisha nchi kushindwa kupiga hatua kiuchumi.

Alisema sasa ni wakati Watanzania kuwa wa moja, kushikamana na kufutana machozi, hivyo wanatarajia kwa Rais Samia kushirikiana na viongozi wenzake wataijenga vizuri nchi na kuiweka kwenye mpangilio mzuri.

HABARI KITAIFA

# Kasi ya Samia yamwibua mbunge

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa Morogoro Mjini (CCM), Abdulaziz Abood, amepongeza kasi ya Rais Samia Suluhu Hassan na kueleza kuwa ameonyesha nia ya dhati kuleta maendeleo ya kweli.

Kutokana na kasi hiyo, amewaomba Watanzania wote bila kujali itikadi zao, kumuunga mkono na kumwombea atekeleze majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuendeleza miradi ya kimkakati na kuinua uchumi kwa Watanzania.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na gazeti hili kuhusu kasi nzuri aliyoanza nayo Rais Samia mara tu baada ya kuapishwa kuwa Rais wa sita wa Tanzania.

Mbunge huyo alisema kasi aliyoanza nayo Rais Samia ni nzuri na imewapa matumaini makubwa Watanzania kwamba atafanya kazi kubwa ya kuinua uchumi na kupiga vita vitendo vya rushwa na ufisadi katika uongozi wake.

"Sisi Watanzania tuwe kitu kimoja bila kujali huyu ni chama gani huyu ana itikadi gani. Tumuunge mkono Rais wetu kwa sababu ana nia njema ya kuleta maisha bora kwa Watanzania," alisema.

Hatua ya Rais Samia kumwagiza Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kuchunguza fedha zilizotumika kati ya Januari na Machi mwaka huu, alisema ni ushahidi tosha wa namna alivyo na dhamira ya dhati ya kuhakikisha analinda fedha za umma na kukomesha wizi.

Alisema Rais Samia ana uzoefu wa kutosha kwa kuwa amekuwa Waziri kwa muda mrefu kabla ya kuwa Makamu wa Rais kwa muda wa miaka mitano, hivyo itakuwa rahisi kwake kuiongoza nchi kwa weledi. "Rais Samia tulikuwa naye kwenye Bunge la Katiba akiwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge hilo, hivyo tunajua uwezo wake mkubwa wa kuchambua mambo na kiuongozi ni mtu ambaye huwezi kuwa na shaka naye hata kidogo," alisema Abood. Pia alisema hotuba yake aliyoitoa juzi baada ya kuwaapisha mawaziri na naibu mawaziri ya kuikaripia Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), imezidi kukonga nyoyo za Watanzania kwa kuwa wengi waliifurahia na kuiona imejaa hekima na busara.

Kwenye hotuba hiyo, Rais Samia aliiambia TRA itumie akili zaidi badala ya kutumia mabavu na vitisho kwa wafanyabiashara wakati wa kukusanya kodi.

Rais Samia alisema mazingira hayo yamewafanya baadhi ya wafanyabiashara kufunga biashara na kwenda kuwekeza kwenye nchi zingine hali inayoikosesha serikali mapato.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, akionyesha kwa waandishi wa habari jana, ngozi za wanyama, bunduki aina ya gobore na kifurushi cha bangi, vilivyokamatwa na jeshi hilo, katika operesheni inayofanyika kipindi hiki cha kuelekea sikukuu ya Pasaka. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kilio cha vifurushi, gharama za simu chatawala kila kona

**Na Mwandishi Wetu**

MABADILIKO ya vifurushi vya huduma ya mtandao yaliyofanywa na kampuni za simu ya mkononi jana ilizua tafrani kwa watumiaji, huku wengi wakilalamika hakuna unafuu wowote.

Kwenye mitandao ya kijamii, wananchi wengi walionyesha kuwa na ghadhabu huku baadhi yao wakieleza kuwa mabadiliko hayo yamelenga kunyonya mtumiaji.

Pia baadhi yao walilalamika mabadiliko ya bei za vifurushi hivyo badala ya kupungua kama ilivyotangazwa awali na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), vimeendelea kuwa juu na kuwaumiza.

Desemba 29, mwaka jana, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, aliipa miezi mitatu TCRA, kumaliza malalamiko ya vifurushi yanayotolewa na wateja dhidi ya kampuni za simu.

Ndugulile pia aliitaka TCRA ishughulikie malalamiko ya wananchi kwa kuwa hawana imani na vifurushi na 'bando'.

Waziri pia aliitaka kuhakikisha kunakuwapo na mfumo wa kuhakiki gharama halisi za mawasiliano kuendana na fedha aliyotoa mteja na kuwe na namba ya bure ambayo wananchi watapiga ili kuwasilisha malalamiko yao waweze kuwa na imani na serikali yao.

Ndugulile aliitaka TCRA kushirikiana na Baraza la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA - CCC), kumaliza tatizo hilo kwa maelezo kuwa Watanzania si wajinga.

Hata hivyo, jana katika kutekeleza mwongozo wa kanuni za TCRA, kampuni za simu zilazimika kushusha kifurushi na kuacha fedha za ununuzi kama ilivyokuwa awali au kuacha kiwango cha fedha na kushusha kifurushi cha awali.

Machi, mwaka huu, TCRA ilitoa mwongozo wa kanuni ndogo ya 12 zinazolenga kutatua kero za watumiaji wa huduma za simu, ikiwamo matumizi ya vifurushi ambazo walitangaza kuanza kutumika rasmi Aprili Mosi, mwaka huu.

Hatua hiyo, ilitokana baada ya mamlaka hiyo kupokea maoni 3,278 ya malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali ikijumuisha watumiaji, watoa huduma, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ili kutatua kero na kuongeza ustawi wa sekta ya mawasiliano.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, James Kilaba, aliwaambia waandishi wa habari siku hiyo kuwa kwa kuzingatia maoni na ushauri wa wadau, mamlaka hiyo imeandaa kanuni hizo ikiwamo ya mtoa huduma hataruhusiwa kutoa ama kufanya shughuli hizo bila kibali cha mamlaka.

Kilaba pia alitaja kanuni nyingine kuwa ni mtoa huduma ataweka utaratibu wa kumwezesha aliyejiunga na kifurushi chochote, kuendelea kutumia muda au uniti za kifurushi ambacho kitakuwa kimesalia ndani ya muda wa matumizi uliowekwa kwa kununua tena kifurushi hicho kabla ya kumalizika muda wake.

Vilevile alisema mtoa huduma ataweka utaratibu au mfumo wa kumwezesha mtumiaji wa huduma kuhamisha uniti za kifurushi kwenda kwa mtumiaji mwingine ndani ya mtandao wake kwa masharti yaliyopo.

# Askofu akemea ubinafsi uroho wa madaraka

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dodoma, Beatus Kinyaiya, amewataka Watanzania kuacha tabia ya ubinafsi, uroho wa madaraka na ubadhirifu wa mali.

Pia amewahimiza Watanzania kumwombea Rais Samia Suluhu Hassan ili kutoa suluhu ya matatizo yanayowakabili kutokana na hotuba zake alizozitoa hivi karibuni kuonyesha mwanga.

Akihubiri jana katika Ibada ya Ijumaa Kuu iliyofanyika katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Paulo wa Msalaba, ambayo ilihudhuriwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, Askofu Mkuu Kinyaiya alisema kanisa litafanya maombi ya kuwaombea viongozi ili taifa liendelee kupata maendeleo kwa amani.

Alisema licha ya viongozi kupiga kelele kuhusu vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa mali za umma, bado watu wamekuwa wabishi sana kuachana navyo.

"Leo (jana) tutafanya maombi ya kuwaombea viongozi wakuu wa taifa, akiwamo Rais Samia Hassan ili atupe suluhu ya changamoto zetu kama ilivyo jina lake, lakini ni mama ambaye tunamfahamu amefanya kazi kwa miaka mitano na hivi karibuni katika hotuba zake, tumeona zinatoa mwanga kwenye taifa letu.

"Makamu wa Rais (Dk. Mpango), sisi viongozi wa dini imekuwa nadra sana kulisema hili lakini ngoja leo niseme hili ni chaguo la Mungu. Amekuwa akipambana kwenye masuala mbalimbali yakiwamo ya rushwa na kama jina lake lilivyo Mpango tunaamini ataweka mipango mizuri kwa ajili ya taifa letu," alisema.

Aidha, aliwasisita kumwombea Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ili viongozi hao wa juu wafanye kazi kwa utatu ambao utasaidia taifa kupiga hatua.

Kuhusu suala la usaliti, askofu huyo alisema limeendelea kukua ndani ya jamii.

"Usaliti upo kwenye ndoa, viongozi, wananchi kulisaliti taifa lao, lakini wakristo kujisaliti kwa kushindwa kuishi kwenye misingi ya kikristo. Ipo haja ya wakristo kuona fahari ya ukristo wao hadi wazazi kuna majina wanaita watoto haijulikani kama ni mkristo au mwislamu," alisema.

Naye Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Dodoma, Amon Kinyunyu, aliwataka Watanzania kuitumia siku hiyo kumwombea Rais Samia ili aongoze kwa amani. Akihubiri ibada ya Ijumaa Kuu katika Kanisa la KKKT, Usharika wa Arusha Road jijini hapa, Askofu Kinyunyu alisema ni wajibu wa Watanzania kuendelea kuliombea taifa na familia ili amani izidi kuwapo.

"Tunajua kuwa tuna maombolezo ya kuondokewa na aliyekuwa Rais wetu Hayati Dk. John Magufuli, hivyo Ijumaa Kuu hii itukumbuke kumwomba Mungu azidi kuilinda amani ya nchi yetu na kuziombea familia zetu," alisema.

Alisema pamoja na kuondokewa na kiongozi huyo, lakini Mungu amemwinua Rais Samia katika kuliongoza taifa, hivyo anahitaji kuombewa ili azidi kuongoza kwa amani na mafanikio.

"Tumeona jinsi Rais Samia alivyoanza kazi, mimi nilivyokuwa nikimsikiliza kwenye hotuba zake, nimeona ameanza kazi kama alivyoanza Hayati Magufuli kwa sababu alianza na kuwatumbua watu na yeye juzi ameanza hivyo," alisema.

Kadhalika alisema Rais Samia ameonyesha kuwa mchapakazi na atakuwa tayari kuwatetea wanyonge kutokana na kuanza kuteua wasaidizi wake katika serikali ambao anaamini wataendana na malengo ya nchi yaliyokusudiwa .

**Imeandaliwa na Paul Mabeja, Ibrahim Joseph, na Peter Mkwavila (DODOMA)**

## Wachanga fedha kujenga zahanati

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI wa kijiji cha Nyaligongo wilayani Shinyanga, wanaojishughulisha na uchimbaji wa dhahabu, wamejitolea kuanza ujenzi wa zahanati ili kuondokana na adha ya kufuata huduma ya matibabu umbali mrefu.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Masumbuko Lushona, aliyasema hayo juzi katika ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, ambaye alifika kukagua ujenzi wa zahanati hiyo.

Mwenyekiti huyo alisema baada ya kuona wanapata shida ya matatibu, walichangishana fedha ili kuanza ujenzi.

Alisema wananchi wa kijiji hicho hufuata huduma ya matibabu umbali wa kilomita tano katika kijiji jirani cha Mwakitolyo, huku baadhi ya kinamama wakijifungulia njiani. Alisema kukamilika kwa zahanati hiyo kutawaondolea changamoto hizo na kuimarisha afya zao.

"Wakazi wa kijiji hiki cha Nyaligongo shughuli zao kubwa ni uchimbaji wa madini ya dhahabu, hivyo hatushindwi kujenga zahanati. Sasa tuko katika hatua ya msingi na hadi kufika mwishoni mwa mwaka huu itakuwa imeshakamilika. Makisio yetu itagharimu Sh. milioni 90," alisema Lushona.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Hoja Mahiba, aliwapongeza wananchi hao kwa kuanzisha ujenzi wa zahanati na kubainisha kuwa sera ya afya inasema kuwapo na zahanati kwa kila kijiji. Alisema miradi hiyo huibuliwa na wananchi wenyewe kisha serikali inawaunga mkono kuikamilisha.

Kwa upande wake, Mboneko alisema ni jambao jema wananchi hao kujitolea kuchangia shughuli za maendeleo kwa kutatua changamoto zao kuliko kuitegemea serikali kwa kila kitu.

Mkuu huyo wa wilaya aliahidi kuwaunga mkono hadi zahanati hiyo itakapoanza kutoa huduma za matibabu.

Baadhi ya wanawake wa kijiji hicho akiwamo Mary Benjamini, walisema ujenzi wa zahanati hiyo utakuwa msaada kwao na kwamba huduma za matibabu zinapokuwa mbali wanaoteseka huwa ni wanawake na watoto.

# Mwenyekiti wa mtaa afa kwa kuchomwa na kitu cha ncha kali

**Na Samson Chacha,** TARIME

WATU wawili wamefariki dunia katika Kata ya Sabasaba mjini Tarime katika matukio mawili tofauti ikiwamo la Mwenyekiti wa Mtaa, Juma Kamugisha, kuchomwa na kitu chenye ncha kali tumboni akiwa katika doria.

Tukio lingine ni la mlinzi wa duka, Nyamhanga Mwita, kuuawa kwa kukatwa panga wakati akiwa katika ulinzi usiku.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tarime/Rorya, William Mkonda, amethibitisha kutokea kwa matukio hayo na kueleza kwamba Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa matukio hayo na kuwaomba wananchi kutoa ushirikiano.

Wakizungumza na Nipashe kuhusu kifo cha Kamugisha, Katibu Mwenezi wa CCM Wilaya ya Tarime, Malema Solo; Diwani wa Sabasaba, Leonard Balenzo, Mdogo wa Marehemu, Shaban, walisema wamempoteza kiongozi mchapakazi. Walisema Kamugisha wakati wa uhai wake alijitolea kutumikia na kuitetea Ilani ya CCM kwa vitendo, alipambana na uhalifu, alitatua migogoro katika jamii.

Shaban alisema kaka yake siku ya tukio alikuwa doria na wenzake katika mtaa wa Kibasa jirani na baa ya Kebacho. Alisema walipokuwa katika eneo hilo, walikutana na kundi la vijana na walipowasimamisha kutaka kuwahoji ghafla ndugu yake alichomwa na kisu tumboni na mmoja wapo wa vijana waliosimamishwa.

"Alipiga kelele kwa kuomba msaada kwa wenzake huku waliotekeleza tukio hilo wakikimbia bila kukamatwa. Alipelekwa Hospitali ya Wilaya ya Tarime kwa matibabu kisha Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mara, Musoma, baadaye ambako alifariki dunia," alisema.

Katika tukio la pili, mtaa huo huo wa Sabababa mlinzi wa duka la nguo katika Soko la Serengeti mjini, Mwita, aliuawa usiku kwa kukatwa panga na watu wasiojulikana waliokuwa wamebeba silaha za jadi, kisha kupora nguo zilizokuwamo katika duka hilo.

Akizungumza na Nipashe, kaka wa marehemu, Chacha Ghati, alisema ndugu yake alikuwa mlinzi katika maduka kwenye Soko la Serengeti.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, akizungumza na menejimenti ya ofisi hiyo, jijini Dodoma juzi, baada ya kuapishwa na Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: AUGUSTA NJOJI**

# Rais Samia apongezwa kwa kukumbuka maendeleo jamii

**Na Raymond Mushumbusi,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza nguvu katika wizara hiyo hasa kwa kuzingatia sekta ya maendeleo ya jamii.

Dk. Gwajima aliyasema hayo jijini Dodoma juzi, wakati akizungumza na watumishi wa wizara hiyo wakati wakimkaribisha Naibu Waziri anayeshughulikia Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamis.

Dk. Gwajima alisema Idara ya Maendeleo ya Jamii ni kitovu cha maendeleo ya taifa na kama sekta hiyo na ya ustawi wa jamii zitasimamiwa vizuri, sekta zingine zitapata ufanisi, hivyo kuharakisha maendeleo kwa taifa zima.

"Sekta ya maendeleo ya jamii ni mbeleko ya maendeleo ya taifa na ni muhimu sana katika kuchangia sekta zingine kuendelea na kukua katika kusaidia maendeleo ya taifa kwa ujumla," alisema Dk. Gwajima.

Aliongeza kuwa masuala ya maendeleo ya jamii yakikaa sawa matatizo mengi yanayowakumba wananchi kama vile magonjwa hayatapata nafasi.

Pia alisema jamii ikielimika itatatua changamoto zinazoikabili kutokana na elimu aliyoipata kutoka kwa wataalamu wa maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii.

"Katika sekta ya maendeleo ya jamii ikitumika ipasavyo watu wakaelimika na kujua vitu vingi wataondokana na changamoto zinazowasibu ambazo zinatatulika," alisema Dk. Gwajima.

Katibu Mkuu Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, alimhakikishia kufanya kazi kwa kushirikiana ili kuhakikisha matokeo na matarajio ya Rais Samia yanafikiwa.

Alisema maendeleo ya nchi yanahitaji ubunifu na matumizi ya teknolojia na mabadiliko ili kuhakikisha wananchi wanabaki nyuma.

Aliongeza kuwa hatua ya Rais Samia kumteua naibu waziri anayeshughulikia maendeleo ya jamii ni ya kujivunia sana na jambo linalofuata ni kuhakikisha maono ya Rais yanatafsiriwa kwa vitendo.

Akizungumza baada ya kukaribishwa, naibu waziri huyo alisema atafanya kazi kwa ustadi na kwa kasi ili kuhakikisha sekta anazosimamia zinakuwa na maendeleo na kutoa matokeo chanya na yanayonufaisha jamii.

# Wachimbaji wadogo hatarini kukosa ajira

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

IDADI kubwa ya wachimbaji wadogo wa dhahabu katika machimbo ya Mpipiti, wilayani Singida, wako hatarini kupoteza ajira zao endapo serikali itaendelea kuzuia uchenjuaji kwa kutumia mercury.

Hayo yalibainishwa juzi na wachimbaji hao walipokuwa wakizungumza na waandishi wa habari waliotembelea, kukagua na kufahamu changamoto zinazowakabili.

Mmoja wa wachimbaji hao, Mussa Maduhu, alisema wamekuwa wakitumia gharama kubwa kuchimba kutokana na kutumia mafuta aina ya dizeli baada ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Singida kushindwa kuwapelekea umeme kwenye machimbo hayo.

Alisisitiza kwamba kutokana na wamiliki wa migodi hiyo kutumia gharama kubwa kuliko mapato yanayotokana na shughuli hizo, watalazimika kuwapunguza wafanyakazi ili kubaki na watu wachache watakaoendana na gharama zinazopatikana.

"Lakini kilio kikubwa hapa tuna maduara zaidi ya 200 hawa watu wote wanategemea ajira kwenye yale mashimo. Kama walivyosema wenzangu kuhusu umeme, alishakuja mkuu wa wilaya hapa, alishakuja DAS (Katibu Tawala wa Wilaya) hakuna kilichofanyika," alisema.

Maduhu alionesha kukerwa na baadhi ya madalali walioko katika ofisi za madini Singida wanaonunua dhahabu kutokana na kushusha thamani ya dhahabu.

Alisema dhahabu iliyoko katika machimbo hayo ina asilimia 84 mpaka 90 lakini inapofika na kuchomwa inafika asilimia 62, kitu ambacho kinaonesha wachimbaji wadogo wanaibiwa na wanunuzi hao.

Fadhili Iddi, mmoja wa wachimbaji wadogo, aliweka bayana kwamba wanaofahamika kuwa wao ni wachimbaji wadogo, hivyo endapo matumizi ya zebaki yataondolewa, hawatakuwa na uwezo wa kumudu gharama zinazotakiwa kutekelezwa wakati wa uchenjuaji huo.

Aliishauri serikali kuangalia upya uamuzi wa kuzuia zebaki kwa kuwa wao ni wataalamu, wamesoma na wanajua madhara yake, hivyo waangalie uwezekano wa kuwapatia vifaa mbadala vitakavyowakinga na madhara hayo kutokana na kutumia zebaki.

Kaimu Ofisa Madini Mfawidhi Mkoa wa Singida, Lucy Kimaro, alisema wachimbaji wa madini wana kipimo uzito wa dhahabu peke yake na kukanusha kwamba hawana kipimo cha kuonyesha ubora wa dhahabu.

# Waomba Samia, Kenyatta kutatua mgogoro mahindi yaliyokwama

**Na Asraji Mvungi,** LONGIDO

WASAFIRISHAJI na wafanyabiashara wa mahindi waliokwama katika mpaka wa Namanga, wamelalamikia kuendelea kupata hasara kutokana na zuio lililowekwa na Kenya.

Kutokana na hasara hiyo kuathiri mitaji yao, wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan na mwenzake Uhuru Kenyatta wa Kenya, kumaliza tatizo hilo kwa kuwa linawaongezea umaskini.

Walielekeza kilio hicho juzi wakati wa kikao cha wadau wa biashara kilichoandaliwa na Baraza la Biashara la Afrika Mashariki. Kikao hicho kilifanyika katika Kituo cha Forodha cha Namanga.

Mmoja wa wadau hao ambaye ni mwakilishi wa Chama cha Wasafirishaji Mizigo cha Kenya, Mercy Ireri, aliomba pia Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kuingilia kati tatizo hilo.

"Tatizo hili ambalo liko nje ya uwezo wetu, linawasababishia hasara wafanyabiashara wa mahindi zaidi ya Dola 200 za Marekani kila siku. Tunaomba sasa wakuu wa nchi hizi mbili wakae pamoja na kuja na suluhu," alisema.

Ireri alisema pamoja na wataalamu wa serikali ya Kenya kuchukua sampuli za mazao yao, kwa lengo la kwenda kupima kama zina sumukuvu ama laa, hadi sasa hawajatoa majibu yeyote na kila wanapouliza hawapati majibu.

Kukwama kwa wafanyabiashara hao wa mahindi kulitokana na serikali ya Kenya kuyazuia malori yenye shehena ya mahindi kutoka Tanzania kuingia nchini humo, hali iliyoibua taharuki na malalamiko makubwa katika mpaka wa Namanga.

Akijibu malalamiko hayo, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Chakula na Kilimo wa Kenya, Cacutus Efukho, alisema uchunguzi wa sampuli hizo unaendelea na wakati wowote taarifa itatolewa.

Naye Mshauri wa Biashara na Sera wa Baraza la Biashara la Afrika Mashariki, Adrian Njau, alisema mapendekezo ya wadau wa pande zote yatafikishwa kwenye ngazi zinazohusika.

Machi 5, mwaka huu, serikali ya Kenya ilitangaza kuzuia mahindi kutoka Tanzania kuingia nchini humo.



TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

PONGEZI

MHE. MHANDISI HAMAD YUSSUF MASAUNI



*Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), tunakupongeza, **Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni** kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. Tunakutakia mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yako kwa maendeleoya Taifa letu.*

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la heri Simba katika Ligi ya Mabingwa Afrika

**WAWAKILISHI** wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba ya jijini Dar es Salaam wanatarajia kushuka dimbani kuwakaribisha wapinzani wao, AS Vita kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Mechi hiyo itakayochezwa kuanzia saa 10:00 jioni ni ya mzunguko wa tano na itakuwa ni mchezo wa mwisho nyumbani katika hatua hiyo ya makundi kwa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Simba ambao wana pointi 10 na wanaongoza katika msimamo wa Kundi A lenye timu nyingine mbili ambazo ni Al Ahly ya Misri na Al Merreikh ya Sudan, inahitaji pointi moja tu ili isonge mbele katika mashindano hayo yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Tangu mwaja juzi, Wekundu wa Msimbazi wamekuwa na rekodi nzuri katika mashindano hayo ya kimataifa wanapocheza kwenye uwanja wa nyumbani, lakini msimu huu wameonekana pia bora kwa kuvuna pointi walipocheza ugenini Kinshasa, DRC na Khartoum.

Nipashe inaungana na wadau wengine wa michezo kuiombea dua njema Simba ili bendera ya nchi iendelee kupeperushwa vizuri katika mashindano hayo kwa kuondoka na ushindi katika mechi ya leo au sare ya aina yoyote na hivyo itakuwa imekamilisha hesabu zake.

Watanzania wanatakiwa kuungana kuhakikisha wawakilishi hawa wanapata matokeo chanya katika mechi hii ili kujiondoa kwenye presha ya kusaka ushindi watakapokwenda ugenini ambapo pia wenyeji wao watakuwa wamejipanga kulipiza kisasi cha kufungwa katika mchezo wa kwanza.

Hata hivyo, baada ya mechi ya leo, Simba itasafiri kuelekea Cairo kuwafuata wenyeji wao mabingwa wa zamani wa Afrika, Al Ahly kwa ajili ya mchezo wa mwisho wa kukamilisha hatua ya makundi utakaochezwa wiki ijayo.

Ili kujiweka katika nafasi salama zaidi, Simba na Watanzania leo wanatakiwa kuondoka na matokeo chanya kwa sababu watajihakikishia moja kwa moja tiketi ya kutinga hatua ya robo fainali na hivyo kujiondoa kwenye sintofahamu kwa kusubiri matokeo ya mechi ya mwisho.

Huu ni wakati wa mashabiki na wadau wa michezo kuweka tofauti zao pembeni kwa sababu Simba inasimama kama mwakilishi wa Tanzania na kusonga kwake mbele kutaifaidisha nchi kwa kutoa timu nne katika mashindano ya CAF kwenye msimu ujao.

Pia kutaifanya TFF ambayo ni mwanachama wa CAF kupata bonasi kutokana na mafanikio hayo ya Simba kwenye michuano hiyo kama ilivyokuwa msimu wa mwaka juzi.


Nipashe tunapenda pia kuwakumbusha wachezaji wa Simba kuendelea kujituma katika mechi ya leo na ya mwisho kwa sababu kwa kufanya hivyo kutawaweka sokoni kupitia mawakala mbalimbali wanaoifuatilia timu yao.

Wachezaji wa Simba wafahamu ndoto za kwenda kucheza soka la kulipwa linaweza kutimia kupitia michuano hii msimu huu kama ambavyo ofa kutoka kwa klabu zaidi ya tano zimetua kwa Wekundu wa Msimbazi zikihitaji huduma ya golikipa wake chaguo la kwanza, Aishi Manula.

Viongozi, wachezaji na mashabiki huu ni wakati mwingine wa kila mmoja kuhakikisha anatimiza majukumu yake kwa kiwango cha juu na kumuenzi vyema aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Pombe Magufuli kwa kupata ushindi ambao utakuwa ndani ya siku 21 za maombolezo.

Hakuna kisichowezekana, kama klabu nyingine zimekuwa na mafanikio ya kucheza robo fainali kila mwaka, msimu huu uwe wa mafanikio zaidi kwa Simba ambayo ina deni la kuleta kikombe cha Afrika na kumaliza unyonge wa timu kutoka Kanda ya Afrika Mashariki kwenye michuano hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# Udugu wa nazi hukutania chunguni

**UDUGU** wa nazi ni kukutana katika chungu. Methali hii hutumiwa kuwatolea mfano watu wasioweza au wasiopenda kushirikiana hadi inapokuwa wakati m-baya sana na wanapokuwa wamechelewa. Yafaa kutambua faida ya kushirikiana mapema.

Shabiki wa Yanga aitwae Ladislaus Kalugaba aliandika hivi kwenye safu ya "Maoni ya Mashabiki" yanayochapishwa na gazeti la Mwananchi ukurasa wa 6 Jumanne iliyopita: "Mi ni Yanga ila... niko pamoja na mashabiki wa Simba kuwaombea ushindi katika mchezo dhidi ya AS Vita."

Mwingine aitwae Isaya Jeremia aliandika kwenye safu hiyo kwamba: "Naipenda sana timu yangu ya Yanga lakini wanatuangusha. "Ina mastaa kibao lakini wafungaji tu ndio wanaotuangusha."

Msomaji wa makala zangu katika safu hii ya "Muugwana Lazima Nilonge" aliniandikia yafuatayo: "Naitwa Mussa Lima. Mimi ni mfuatiliaji sana wa makala zako lakini tatizo la Simba na Yanga, wasemaji ndio wanaochochea mpasuko wa timu hizi mbili ilhali zamani hayakuwepo.

"Kwa asilimia 90 huwa sifurahii na maneno ya wasemaji wa timu za SIMBA na YANGA. Hawa ndio wanaoharibu mpira wetu kwa sababu wanahubiri chuki na sio kusemea timu zao mambo ya msingi."

Ni kweli kwamba baadhi ya mashabiki na wanachama wa Simba na Yanga wakiwamo viongozi hawapendi kuona moja- wapo ya timu hizi ikiwa na maendeleo mazuri inapopambana na timu kutoka nje ya Tanzania!

Wahenga walisema: "Ndugu mbaya humshinda rafiki mzuri." Maana yake hata rafiki akawa mzuri kiasi gani hawezi kuwa sawa na ndugu yako hata akawa m-baya.

Tunakumbushwa umuhimu wa kuwathamini ndugu zetu au watu tulio na ujamaa nao kwa kuwa wanaweza kutufaa kuliko wanavyoweza kufanya marafiki zetu.

"Chuki humchoma anayeihifadhi." Maana yake kwa kawaida chuki humsumbua anayeiweka au kuihifadhi chuki hiyo. Methali hii inatufunza umuhimu wa kutoiweka chuki kwa kuwa tunajidhuru wenyewe.

Biblia Takatifu yasema: "Yeye asemaye kwamba yumo nuruni, naye amchukia ndugu yake, yumo gizani hata sasa. Yeye ampendaye ndugu yake, akaa katika nuru, wala ndani yake hamna kikwazo. Bali yeye amchukiaye nduu yake, yu katika giza, tena anakwenda katika giza, wala hajui aendako, kwa sababu giza limempofusha macho." (1Yohana 9:11).

"Hivi ndivyo zilivyo Simba na Yanga ambazo mashabiki na hata baadhi ya viongozi wao pia ndivyo walivyo. Salala (tamko linalodhihirisha hisia ya mshangao)!

"Tazama, jinsi ilivyo vema, na kupendeza ndugu wakae pamoja, kwa umoja. Ni kama mafuta mazuri kichwani, yashukayo ndevuni, ndevu za Haruni, yashukayo mpaka upindo wa mavazi yake. Kama umande wa Hemoni ushukao milimani pa Sayuni maana ndiko Bwana alikoamuru Baraka, naam, uzima hata milele." (Zab.133:1-3).

"Busara itangulie kila kazi, na mashauri yatangulie kila tendo. Shina la mashauri yatangulie kila tendo. Shina la mashauri ya moyoni huchipuza matawi manne; mema na mabaya, uzima na mauti, na daima mtawala wake ni ulimi." (Yoshua bin Sira 37:16-18).

Jumamosi ya leo, Simba inayoiwakilisha Tanzania kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, itapambana na AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Jijini Dar es Salaam. Twapaswa kuishangilia Simba kwa bidii kwani inawawakilisha Watanzania wote wakiwamo Yanga, mimi nikiwa mmoja wao.

Tuache ujinga na chuki Simba au Yanga zinapopambana na timu ngeni kwani kufanya hivyo tunajionyesha jinsi tulivyo wajinga, kwani " Ujinga wa kuuza si ubaradhuli (upumbavu) wa kununua."Ni heri kuwa mjinga wa kuuza kuliko kuwa mjinga wa kununua.

Kesho Jumapili timu yetu ya Namungo FC itapambana dhidi ya Nkana kutoka Zambia hapa jijini pia. Twapaswa kuishangilia kwa bidii timu yetu ya nyumbani.

Asiyependa kuzishangilia Simba na Namungo ni mchimvi, yaani mtu anayesababisha balaa kwa watu wake tena ni mzabizabina yaani chakubimbi!

**marobarnabas@yahoo.com 0784-334 096**

## HABARI KITAIFA

# Wapinga vijiji kuingizwa katika hifadhi

**Na Thobias Mwanakatwe,** KISARAWE

WANANCHI wa vijiji vya Mtunani, Kitonga Chole na Panga la Mwingereza, Kisarawe mkoani Pwani, wamepinga upimaji upya ardhi ambao utavifanya kuingizwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere (Selous).

Walitoa msimamo huo jana kwenye mkutano wa viongozi wa serikali za vijiji vinavyopakana na hifadhi hiyo ambao ulikuwa maalum kujadili mgogoro wa mpaka ambao umetokana na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) kuanza kumega maeneo ya ardhi ya vijiji hivyo na kuviingiza kwenye hifadhi bila kushirikisha wananchi.

"Tunapinga na tunataka upimaji ardhi usitishwe haraka na Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii na Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi wafike kwenye vijiji vyetu wasikilize kilio chetu," alisema Amin Juma wakati akisoma maazimio ya mkutano mbele ya maofisa kutoka wizara hizo ambao walitoka Dodoma.

Alisema upimaji mpya wa ardhi katika vijiji vyao unakiuka sheria, kanuni na taratibu kwa kuwa haujazingatia mipaka ya asili kati ya hifadhi na vijiji husika. Pia alisema unafanywa katika maeneo yaliyopimwa na kupangiwa mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Naye Diwani wa Vikumburu ambaye alikuwa mwenyekiti wa mkutano huo, Siri Gongo, alisema mgogoro wa ardhi katika vijiji hivyo umekuwa wa muda mrefu kutokana na wizara husika kuchelewa kupatia ufumbuzi. Alisema hali hiyo inakwamisha maendeleo kutokana na wananchi kushindwa kuendelea na shughuli za kilimo.

"Tuna imani kubwa na mawaziri wa wizara zinazowajibika katika kuutafutia ufumbuzi mgogoro huu. Kwa hiyo tunawaomba wachukue hatua haraka ili wananchi waendelee na kilimo ambacho ndiyo tegemeo lao katika kuendesha maisha yao ya kila siku," alisema.

Naye Gasper Matovu, Katibu wa Kikundi cha Wakulima walioathirika baada ya kukamatwa na askari wa TAWA, alisema maofisa ardhi kutokana wizarani walishawahi kufika katika vijiji hivyo na wanakijiji waliwaomba waonyeshe mipaka inayotokana na ramani iliyopo lakini walikataa kufanya hivyo kwa sababu wanajua kupitia ramani hiyo inayotambulika kisheria, vijiji hivyo haviko ndani ya hifadhi.

Alisema mgogoro huo wa ardhi umesababisha mkazi wa kijiji cha Kitonga Chole Mbwana Telenga (48) kupigwa risasi na kujeruhiwa vibaya na askari wa TANAPA Agosti 9, mwaka jana.

Mwananchi mwingine, Mosty Mwasenga, alisema mgogoro huo umekuwa kero kubwa kwa kuwa Februari, 2019 wakulima wanane walikamatwa na askari wa TAWA na kufunguliwa kesi namba 55/2019 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Morogoro kwa madai kuwa walikuwa wakilima ndani ya hifadhi.

Hata hivyo, upelelezi wa kesi hiyo ulipofanyika ilibainika kuwa walikuwa wakilima kwenye eneo halali la kijiji na si hifadhi hali iliyomfanya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuiondoa kesi hiyo Julai 29, 2019.

Aidha, vifaa vya wakulima kama matrekta mawili, jembe, mbegu na vingine vilivyokuwa vimekamatwa na TAWA vilirejeshwa na kukabidhiwa kwa wakulima Februari 11, mwaka huu, ikiwa ni miaka miwili tangu vilipokamatwa.

Maofisa kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kitengo cha upimaji waliohudhuria mkutano huo, walisema suala hilo watalifikisha kwa uongozi wa juu wa wizara ili waangalie hatua zaidi za kuchukua.

# RPC awaonya watakaofanya fujo Pasaka

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Dodoma, limewataka wananchi kusherehekea Pasaka kwa utulivu wakiwa nyumbani na kuacha tabia ya kuingia barabarani na kufanya fujo.

Kamanda wa Polisi Mkoa, Kamishna Msaizidi Mwandamizi (SACP) Gilles Muroto, alitoa amri hiyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema katika msimu huu wa Pasaka, jeshi hilo limejipanga kuimarisha ulinzi katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Dodoma.

"Tunaimarisha ulinzi katika msimu huu wa sikukuu za Pasaka katika maeneo mbalimbali pamoja na nyumba za ibada. Tunawaomba watu baada ya kutoka katika nyumba za ibada, watulie nyumbani na si kuingia barabarani," alisema.

Muroto alisema pia jeshi hilo litaimarisha ulinzi katika maeneo ya barabara kwa kuweka vizuizi vya magari yanayoingia na kutoka ndani ya mkoa wa Dodoma.

"Hakuna mhalifu atakayetoka salama baada ya kufanya uhalifu katika mkoa wa Dodoma kutakuwa na vizuizi vya magari katika njia zote," alisema.

**Wakati huo huo,** jeshi hilo katika msako wake limekamata silaha nane aina ya gobore, bangi miche 32, ngozi mbili za digidigi na moja ya kenge na pikipiki saba ambazo zilihusika katika unyang'anyi.


TRA
MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA
Imethibitishwa na ISO 9001: 2015
PONGEZI
MHE. DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA
Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), tunakupongeza, **Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba** kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. Tunakutakia mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yako kwa maendeleo ya Taifa letu.

"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"

# Serikali yapania tatizo la mbegu kuwa historia

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imedhamiria kuzikutanisha Wakala wa Mbegu za Kilimo Tanzania (ASA), Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) ili kujadili na kuweka mkakati wa kitaalamu ili kukidhi mahitaji ya mbegu bora kwa wakulima.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, alisema hayo jana akielezea mikakati ya wizara ya uzalishaji wa mbegu akisema ili kufikia malengo hayo, fedha zote katika bajeti ya miradi mipya ya umwagiliaji itasimamishwa na zitaelekezwa kwenye mashamba ya uzalishaji wa mbegu.

Prof. Mkenda alisema hayo mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake, Dk. Christine Ishengoma iliyotembelea kukagua utendaji kazi wa ASA na TOSCI mjini hapa.

Alisema hatua hiyo inakusudia kuongeza uzalishaji wa mbegu bora nchini kwa ajili ya mahitaji ya wakulima na kuondokana kutegemea mbegu kutoka nje ya nchi.

Waziri Mkenda alisema serikali imeweka kipaumbele kumaliza tatizo la mbegu, hivyo itashirikiana na kamati hiyo katika kulisukuma mbele ili kuona mbegu bora zinazalishwa kwa wingi.

"Sisi wizara tutaweka nguvu kwenye bajeti ili kuakisi vipaumbele vyake na kuiwezesha ASA ipate fedha za kutosha kwa ajili ya kusimamia majukumu yake kikamilifu ya kuzalisha na kusambaza mbegu bora nchini kote na kuhakikisha inaboresha mitambo yake.

"Pamoja na ASA pia tunakusudia kutaongeza fedha kwa TARI na usimamizi ili waongeze utafiti zaidi wa mbegu bora na kipaumbele kingine ni suala la ugani litaboreshwa zaidi," alisema Prof. Mkenda.

Alisema kazi kubwa zimefanyika kwa kuanza kupata mbegu bora nyingi kwa ajili ya wakulima na bajeti ya mwaka huu itaelekeza kwa Taasisi za uzalishaji wa Mbegu hasa ASA na TARI.

Takwimu zinaonyesha kwa kipindi cha miaka minne upatikanaji wa mbegu umeongezeka kutoka tani 36,614 mwaka 2015/16 hadi tani 76,725 mwaka 2019/20, huku uzalishaji wa ndani wa mbegu bora umeongezeka kutoka tani 20,604 mwaka 2015/16 hadi tani 69,173 mwaka 2019/20.

# Wanafunzi 300 wasomea chumba kimoja

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ZAIDI ya wanafunzi 300 wa Shule ya Msingi Kabale, Kata ya Bulyanhulu, Halmashauri ya Msalala, Kahama mkoani Shinyanga, wanasoma katika chumba kimoja kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa.

Shule hiyo ina ya wanafunzi 1,826 huku vyumba vya madarasa vikiwa vinane kati ya 40 vinavyohitajika. Pia chumba kimoja kinatumika kama ofisi ya walimu, ofisi ya mwalimu mkuu, stoo na maktaba.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Elias Kihamba, aliyabainisha hayo jana wakati akipokea mifuko 25 ya saruji kati ya 50 iliyotolewa na Kampuni ya Saruji ya Lake inayotengeneza saruji chapa Nyati, ikiwa jitihada za kuendelea kusaidia kutatua ukosefu wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari wilayani Kahama.

Alisema chumba kimoja kinatumiwa na wanafunzi 300 hadi 350 huku walimu wakipata changamoto ya kufundisha. Idadi inayotakiwa kisheria ni wanafunzi 40 hadi 45 kwa darasa moja.

Alisema katika shule hiyo imekuwa tofauti na kusababisha baadhi ya wanafunzi kushindwa kuelewa kinachofundishwa.

"Darasa la kwanza na pili wanasoma kwa zamu na wale wa awali wanasoma nje ya darasa huku madarasa mengine yaliyobaki wakisomea darasa moja. Pamoja na shule hii kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi, bado imekuwa ikiiongoza katika matokeo ya darasa la nne katika Halmashauri ya Msalala, " alisema Kihamba.

Akikabidhi saruji kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, Ofisa Masoko wa Lake Cement Kanda ya Ziwa, Fadhiri Yustace, alisema kampuni yake imetoa mifuko 50 ya saruji yenye thamani ya Sh. milioni moja ili kuunga mkono serikali katika maendeleo hasa sekta ya elimu.

Akipokea saruji hiyo, Macha alisema itaelekezwa katika Shule ya Msingi Nyahanga iliyoko Halmashauri ya Manispaa ya Kahama na Kabale katika Halmashauri ya Msalala.



Mwezeshaji kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Gemma Akilimali, akiendesha mafunzo kuhusu umuhimu wa kuandaa bajeti yenye mrengo wa kijinsia, kwa wakuu wa idara za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, juzi. Kulia ni Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa halmashauri hiyo, Francisca Makoye. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Ndikilo akabidhi mikopo ya mil. 245.9/-

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amekabidhi vifaa na fedha taslimu vyenye thamani ya Sh. 245,867,100 kama mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Mji Kibaha kwa makundi ya vijana, wanawake na wenye ulemavu.

Vifaa vilivyokabidhiwa ni pikipiki 12, bajaji moja, Toyo moja, mashine ya kutengeneza sabuni na fedha taslim Sh. 177,746,400 kwa vikundi 68 vya wajasiriamali.

Akizungumza wakati wa kukabidhi mikopo hiyo juzi, Ndikilo alisema utoaji mikopo hiyo ni wa kisheria na pia ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 hadi 2025.

Kuhusu utoaji mikopo hiyo na marejesho mkoani hapo, alisema mwaka 2019/20 Sh. bilioni 2.666 zilitolewa kwa vikundi 672 sawa na asilimia 108 ya fedha zilizopangwa kutolewa na marejesho yalikuwa Sh. 645,770,927 sawa na asilimia 54 ya fedha zilizokopeshwa.

Ndikilo alisema kwa mwaka 2020/21, asilimia 10 zilizopangwa na halmashauri zote tisa ni Sh. 2,124,500,000 na hadi kufikia Februari, mwaka huu, fedha zilizokusanywa ni Sh. 1,713,172,068 sawa na asilimia 78.54 ya fedha zilizopangwa na kwamba fedha ambazo zimetolewa kwenye vikundi hadi Februari ni Sh. 1,149,459,447 sawa na asilimia 66.92.

Ndikilo aliziagiza halmashauri zote za mkoa kuhakikisha zinatenga asilimia 10 ya mapato ya ndani na kutoa mikopo kwa wakati na kuacha kutumia fedha hizo kwa matumizi mengine.

Ndikilo alizitaka halmashauri zote mkoani hapo kutoa mkopo hiyo kwa vikundi kwa kuzingatia kanuni, taratibu na sheria zilizopo na kuagiza pia vikundi vikaguliwe na katiba zao kabla ya kupatiwa mikopo.

"Ninataka kuona mikopo hii inasaidia kubadilisha maisha yenu kinamama, vijana na watu wenye ulemavu. Nataka mwelewe kwamba hakuna fedha ndogo, hivyo lazima muwe na mipango thabiti ili fedha ziongezeke na mrejeshe kwa wakati," alisema Ndikilo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Jennifer Omolo, alisema moja ya mafanikio waliyopata katika halmashauri hiyo ni pamoja na kujenga kituo cha biashara katika soko la Mnarani ambacho wajasiriamali wanapata sehemu ya kuuza bidhaa zao.

Omolo aliwataka pia wanawake wajasiriamali kutumia jengo la wajasiriamali lililojengwa katika soko la Mnarani ambalo limejengwa na halmashauri hiyo lakini halitumiki kama ilivyopangwa.



# Waziri aweka mtegoni vigogo TANESCO

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amewapa siku 14 mameneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wa mikoa na wilaya ambao wameshidwa kuwaunganishia umeme wananchi waliolipia kufanya hivyo.

Pia amesema wale walioshindwa kudhibiti kukatika kwa umeme bila sababu ndani ya muda huo nao wataondolewa katika nafasi zao. Dk. Kalemani alibainisha hayo juzi alipotembelea miradi mbalimbali ya umeme katika kata ya Ntyuka jijini Dodoma na kufuatilia utekelezaji wa maagizo aliyoyatoa Januri, mwaka huu.

"Januari 15, nilitoa agizo kuwa nawapa muda wa miezi mitatu mameneja wote wa TANESCO wawe wamemaliza kazi ya kuwaunganishia umeme wananchi waliolipia na hadi leo (juzi) zimebaki siku 14. Wale wote walishindwa wajiandae kufungasha vilago kwenye nafasi hizo," alisema Dk. Kalemani.

Alisema hatakuwa na huruma na meneja ambaye ameshindwa kutekeleza maagizo yake na kuwafanya wananchi waliolipia kuendelea kusota kupata huduma ya umeme.

"Baada ya siku hizi kuisha, tutaonana wabaya kwani walioshindwa kutekeleza agizo hili itabidi watupishe kwani wameshindwa kuzifanyia kazi nafasi zao," alisema.

Pia alisema mameneja ambao wameshindwa kudhibiti matukio ya kukatika kwa umeme katika maeneo yao watawajibika.

"Umeme ulikuwa ukikatika katika kipindi cha nyuma, lakini hivi sasa tumeshamaliza ukarabati wa mitambo yetu yote. Bado kuna maeneo watu wanalalamika kuwa kuna mgawo wa umeme wakati katika awamu hii hatuna mgawo wa umeme. Huo ni uzembe ambao wahusika nikipata orodha yao nitawafungashia vilago," alisema.

Dk. Kalemani alisema pia katika jiji la Dodoma serikali imetenga kiasi cha Sh. bilioni 12, kwa ajili ya kupeleka huduma hiyo katika mitaa yote.

Aliongeza kuwa pia serikali imetoa Sh. bilioni 48 kwa ajili ya maeneo yote ya mkoa wa Dodoma ambayo yanafanana na vijiji yaliyopo katika halmashari ya jiji ambayo wananchi wake wataunganishiwa umeme kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Waziri alisisitiza kuwa katika maeneo hayo yenye sifa za vijiji ambayo yako katika jiji, wananchi wataunganishiwa umeme kwa gharama ya Sh. 27,000 na si vinginevyo.

Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alisema anaishukuru serikali kwa niaba ya wakazi wa mkoa wa Dodoma kwa kuwafikishia huduma hiyo.

"Mweshimiwa waziri tunashukuru sana serikali kwa kutusogeza huduma hii na mimi pamoja na viongozi wa eneo hili tutaendelea kuhamasisha wananchi kulipia na kupata umeme kama ilivyo azma ya serikali," alisema.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (wa tatu kulia), akitoa maagizo kwa Kaimu Meneja wa Shirika la Umeme (TANESCO), mkoa wa Dodoma, Donasian Shamba (mwenye koti la kijani), alipofanya ziara ya kukagua miradi ya umeme katika Kata ya Ntyuka, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Wafurahi TASAF kuboresha maisha yao

**Na Renatha Msungu,** KONGWA

WAJASIRIAMALI wenye ulemavu wa viungo wilayani Kongwa mkoani Dodoma, wameiomba serikali kuendelea na mpango wa kunusuru kaya maskini kutokana na wengi wao umewasaidia kuwainua kiuchumi.

Akizungumza wakati wa ziara ya kutembelea wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini Namhena Mkani, alisema fedha ambazo zinatolewa na TASAF, zimemsaidia kuanzisha biashara ya duka la vinywaji pamoja na ufugaji, hivyo kujiinua kiuchumi.

Mkani ambaye ana ulemavu wa macho, alisema biashara hiyo inamsaidia kujipatia kipato ambacho anakitumia yeye na familia yake.

"Tunaomba mpango wa kunusuru kaya maskini uzidi kuimarishwa kwa sababu umesaidia watu wengi kujikwamua na hali ngumu ya maisha," alisema Mkani. Alisema ana watoto saba ambao anawasomesha kupitia fedha hiyo anayopewa kama ruzuku kutoka TASAF.

Fedha hiyo, alisema ina mchango mkubwa sana kwake kwa sababu imeleta matokeo chanya kwa jamii inayowazunguka.

Pia alisema ufugaji wa kuku na mbuzi anaoufanya, umemsaidia kuendesha maisha yake ya kila siku na amekuwa akiuza baadhi ya mifugo na kununua vifaa vya shule vya watoto.

Alisema alianza na ufugaji wa kuku na baadaye idadi ikaongezeka na kuwa na mifugo mingi ambayo inatokana na uwekaji akiba ya fedha za TASAF.

Naye Mafanikio Richard ambaye ni mlemavu wa miguu alisema fedha za TASAF zimemletea mabadiliko ya maisha yake kutokana na kwamba aliishi maisha ya shida bila kuwa na msaada wowote.

Richard alisema kabla ya kuingizwa katika mpango wa TASAF alikuwa akienda shambani kulima kwa kutambaa kutokana na ulemavu alio nao, lakini baada ya serikali ya mtaa kumwona, ilibaini anastaili kuwamo katika mpango huo wa kupata fedha za kunusuru kaya maskini.

"Naishukuru sana serikali kupitia TASAF kwa kunipatia fedha hizo, niliweka akiba ambayo ilinifanya nianzishe duka na ufugaji wa nguruwe," alisema Richard.

Pia alisema amefanikiwa kuboresha ujenzi wa makazi yake kutoka nyumba ya tembe iliyoezekwa kwa nyasi na badala yake kuweka mabati.

Aidha, aliwata wanufaika wengine kujenga utaratibu wa kuhifadhi fedha wanazopewa na TASAF kwa ajili ya kuanzisha mradi endelevu ambao utawasaidia kujikwamua kimaisha hata pale mpango wa TASAF utakapofikia ukomo.

# Wakulima wanolewa mazao ya kimkakati

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Kituo cha Hombolo, Dodoma, kimetoa mafunzo maalumu kwa wakulima 120, kuhusu mazao ya kimkakati ili kusaidia kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla.

Mafunzo hayo yameleta mwamko mkubwa kwa wakulima kwenye mazao ya kimkakati, hivyo kuwa kichocheo cha maendeleo ya sekta ya kilimo maeneo ya vijijini.

Mkuu wa Kituo hicho, Dk. Lameck Makoye, alibainisha hayo juzi kituoni hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari wakati wa mafunzo hayo kwa wakulima.

"Kwa sasa kuna matumaini kwa kundi hili baada ya kuendesha mafunzo ya mara kwa mara, zikiwamo semina za wazi na mafunzo kwa vitendo," alisema Dk. Makoye

Alisema kutokana na serikali kusisitiza uchumi wa viwanda, kilimo cha mazao ya kimkakati kama vile uwele, mtama na ulezi yanayotumika katika kuandaa baadhi ya vinywaji maeneo ya viwandani, kimepewa kipaumbele.

Pia alisema wamelazimika kuendesha mafunzo kwa wakulima baada ya kubaini kuwa wengi, hususani wa maeneo ya vijijini wanapenda mazao hayo hasa mtama ambao mbali na kutumika kama chakula, pia ni zao la biashara.

"Mazao haya pia yanastahimili ukame na yanachukua muda mfupi ikilinganishwa na mazao mengine," alisema Dk. Makoye.

Diwani wa Chahwa, Sospeter Mazengo, alisema kuna umuhimu wa wakulima wote kushirikiana na TARI, ili walime na kupata tija kwa kuwa na malengo na kutambua faida ya mazao wanayoyalima.

"Pamoja na yote, binafsi nimejifunza kwamba huu mtama una manufaa mbalimbali likiwamo la utengenezaji wa bia. Kama zao la namna hiyo linatengeneza bidhaa inayotambulika dunia nzima, tunaweza kuwashawishi wakulima kutanua wigo ili kuwauzia watu wa viwanda," alisema Mazengo.

Elisha Mwaluko, mkulima kutoka kata ya Ipala Wilaya ya Dodoma, alisema awali walikuwa wanalima kilimo cha kawaida na cha mazoea, kitendo ambacho misimu yote wamebaki kwenye hasara na baa la njaa.

Pia alisema baada ya kushiriki katika mafunzo hayo pamoja na semina mbalimbali, kwa sasa wamebadilika na wanafanya kilimo cha kisasa kwa kuzingatia kanuni.

"Awali kwangu mimi kwenye eka moja ya mtama nilizoea kupata kama kilo 10 hadi 20, lakini kwa sasa naweza kupata mara tano au hata sita ya mazao hayo. Hii imetokana na uelewa wa mafunzo ya TARI, lakini aina ya mbegu tunazotumia sasa," alisema Mwaluko.



# ZSTC: Kuanzishwa kiwanda cha mafuta itakuza uchumi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKURUGENZI wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC), Said Seif Mzee, amesema kuanzishwa kwa kiwanda cha kutengeneza mafuta yanayotokana na majani makavu ya mkarafuu Zanzibar ni hatua mojawapo ya kukuza uchumi.

Aliyasema hayo katika sherehe ya uzinduzi wa Ofisi ya Kiwanda cha Indesso huko Malindi Mjini Zanzibar kinachotengeneza mafuta hayo.

Alisema tayari kiwanda hicho kimeshaanza uzalishaji wa mafuta hayo eneo la Mgelema kisiwani Pemba, kwamba hutumia rasilimali ya malighafi yanayozalishwa Zanzibar ambayo yalikuwa yakipotea ikiwamo majani makavu ya mkarafuu.

Alisema tayari kiwanda hicho kimeshazalisha tani 3.2 za mafuta yatokanayo na majani makavu ya mkarafuu.

Mkurugenzi huyo aliitolea mfano nchi ya Madagasca ambayo inazalisha mafuta kama hayo tani laki moja kila mwaka, kwamba kila tani moja inauzwa Dola za Marekani 10, hivyo endapo Zanzibar nayo ikizalisha tani nyingi itapata faida kubwa.

"Lengo letu ni kuzalisha tani 100 kwa mwaka ya mafuta yanayotengenezwa na majani makavu ya karafuu lakini ili kupata tani hizo ni lazima kuongeza vinu 20 vya uchakataji wa mafuta hayo," alisema.

Aliekuwa Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, alisema kuanzishwa kwa mradi huo serikali haijabahatisha na Zanzibar itapata maendeleo.

Alisema kampuni ya Indesso ni moja ya kampuni iliyokamata soko duniani ikiwamo soko la mafuta ya mchaichai na mafuta mengine yanayotokana na viungo (Spice), hivyo aliwataka vijana wa Zanzibar waitumie fursa hiyo katika kupata ajira na kuongeza kipato.

Akifungua ofisi hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Viwanda, Dk. Islam Seif, alilitaka Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC), kufanya utafiti wa mazao ya viungo mbalimbali vinavyopatikana Zanzibar ili kuongeza uzalishaji wa majani ya miti mengine ya viungo.

Alisema utafiti ni muhimu katika kufanya maamuzi na kuleta matokeo mazuri ya uwekezaji na biashara kwa ujumla.

Alisema ni matumaini ZSTC itaweza kuangalia kwa upeo mkubwa maeneo mengine ambayo yanaweza kupata bidhaa za aina hiyo zinazotokana na malighafi zinazopatikana Zanzibar.

Aidha, aliipongeza kampuni ya Indesso kuongoza katika biashara za mafuta ya viungo vya aina mbalimbali, hivyo ni matumaini yake kuwa ZSTC itapanua wigo na kuongeza uzalishaji Zanzibar ili kusonga mbele kama nchi zengine zinazozalisha mafuta ya viungo ikiwamo Indonesia, Madagasca.

Dk. Islam alisema pamoja na mradi huo lakini wizara inaendeleza jitihada mbalimbali ikiwamo kiwanda cha kusarifu mwani kisiwani Pemba, ili serikali inafikia malengo yake ya kukuza uchumi endelevu.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Indesso Tanzania, Feri Agustian Soleh, alisema uwapo wa taasisi hiyo ni kuimarisha uhusiano wa pamoja kati ya serikali, sekta binafsi na wananchi wa Zanzibar ili kuleta mafanikio kupatikana.

Alisema wameanza uzalishaji wa mafuta ya majani ya karafuu kwa mwaka 2020 tani 3.2 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 50.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Viwanda Zanzibar, Dk. Islam Seif, akikata utepe kuzindua kampuni ya Indesso, huko Malindi, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Asasi zataka upatikanaji vitambulisho kwa usawa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ASASI za kiraia Zanzibar zimeiomba serikali kuhakikisha upatikanaji wa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi (ZAN-IDs) uwe wa usawa na urahisi.

Rai hiyo ilitolewa jana Mjini Zanzibar na Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la Vijana Zanzibar (CYD), Hashim Pondeza, wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu kutetea haki ya wananchi na demokrasia.

Alisema kwa msaada wa taasisi ya Kimataifa ya Demokrasia (NDI) na Shirika la Maendeleo la USAID, asasi nne kutoka Zanzibar, chini ya mwavuli wa ushiriki Tanzania (UT) ilitekeleza kampeni ya miezi mitano kutetea, kushawishi upatikanaji wa vitambulisho hivyo kwa vijana wa Zanzibar, suala ambalo linaonekana ni changamoto kwao.

Alizitaja asasi hizo ni Jukwaa la Vijana Zanzibar (CYD), Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar (JUWAUZA), PIRO na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC).

Alisema kampeni hiyo ambayo ilihusisha udadisi kwa kutumia mbinu mbalimbali, ililenga kuwashirikisha vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kujadili changamoto zao juu ya upatikanaji wa vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi, hasa wakati wa mchakato wa maombi.

Alieleza kuwa katika kukabiliana na hali hiyo, asasi hizo pia zilifanya majadiliano kadhaa ikiwamo kuonana na wanawake na watu wenye ulemavu na kufundisha wasaidizi wa kisheria kutoka Unguja na Pemba, kuwasaidia kufikia vijana zaidi katika ngazi ya chini ili kuwasaidia kuelewa mchakato wa maombi ya upatikanaji wa vitambulisho hivyo.

Alisema wamegundua kuwa vijana wengi, wanawake na walemavu hawajafikiwa kirahisi na kufanikiwa kupata vitambulisho hivyo kwa sababu ya ucheleweshaji wa utoaji wa vitambulisho, kunakosababishwa na urasimu wa masheha.

"Kwa vijana wanaoishi vijijini, imebainika kwamba hawajui vizuri na kwa usahihi upatikanaji juu ya taratibu za maombi na ukosefu wa nyaraka zinazohitajika hasa vyeti vya kuzaliwa na wanawake vijana wanaoishi na ulemavu waliathiriwa zaidi kwani wengi wanakosa vyeti vya kuzaliwa," alisema Pondeza.

Alisema kufuatilia matokeo hayo, asasi hizo za kiraia ziliwasilisha changamoto na mapendekezo kwa wadau na wahusika wa vitambulisho vya Mzanzibari ambao ni pamoja na Waziri wa Tawala za Mikoa na Idara Maalum, Wakurugenzi wa Idara za (ZanID) na vyeti vya kuzaliwa, Mkurugenzi wa Msaada wa Sheria, Mkurugenzi wa watu wenye ulemavu.

# Kesi kuvujwa sheria kudhibiti vileo yaanza kusikilizwa

**Na Mwandishi wetu,** ZANZIBAR

KESI ya kuvunjwa Sheria ya Bodi ya kudhibiti Vileo iliyofunguliwa na Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) imeanza kutajwa Mahakama Kuu Zanzibar mbele ya Jaji Rabia Hussen Maohamed.

Jaji Rabia alisema kesi hiyo itasikilizwa Mei 14 na 19 kwa upande wa waendesha mashtaka wa serikali kujibu hati ya maombi pamoja na kusikiliza pingamizi za awali zitakazo wasilishwa mahakamani na upande wa serikali.

Jaji Rabia alisema mahakama imekubali kutoa muda wa kutosha kwa wanasheria wa serikali ili waweze kujibu hati ya maombi ya walalamikaji wa pamoja na kuwasilisha pingamizi ya awali katika kesi ya msingi.

Kwa mujibu wa hati ya maombi ya walalamikaji Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA), Bodi udhibiti wa Vileo Zanzibar inadaiwa imevunja kifungu cha 33(1) baada ya kutoa vibali vya kuruhusu uingizaji wa pombe kwa kampuni zaidi ya nane badala ya tatu kinyume na Sheria ya Vileo Namba 9 ya mwaka 2020.

Wakili Omar Sheha Omar, alisema sheria imeeleza kuwa: "Kibali cha kuagiza kitatolewa kwa waingizaji wasiozidi watatu kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo; mwingizaji awe Mzanzibar, awe mlipa kodi awe na ghala pamoja na gari ya kusambazia vinywaji.

Alisema kifungu cha 28 (K) kimeweka sharti baa kuanzishwa mbali wa mita 1000 kutoka maeneo ya huduma za jamii kama msikiti, kanisa, shule, hospitali, madrasa lakini bodi imeendelea kutoa leseni bila ya kuzingatia masharti ya kifungu cha sheria.

"Mteja wetu analalamikia Bodi ya Vileo kukiuka kiutendaji na utekelezaji vifungu vya 28(K) na 33(1) ambavyo mteja wetu anaona vifungu hivyo havifanyi kazi ipasavyo kwa kushindwa kuwapa leseni waingizaji watatu kama sheria inavyotaka," alisema Wakili Omary.

Upande wa Bodi ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar unawakilishwa na wanasheria wa serikali kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Abubakary Omar pamoja na Habiba Haji.

Kesi hiyo imehudhuriwa na viongozi 20 wa Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) kutoka Wilaya 11 katika Visiwa vya Unguja na Pemba.

Awali Mwenyekiti wa Bodi ya Vileo Zanzibar, Abdulrazaki Abdulkadiri, alisema aliamua kutoa vibali kwa zaidi ya kampuni tatu kwa kutumia hekima na busara ili kuepusha serikali kupoteza mapato.

Sheria ya Vileo Namba 9 ya Mwaka 2020 ilianza kutumika baada ya kupitishwa na Baraza la Wawakilishi na kusainiwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mei 11, mwaka 2020.



UCHUMBA DAVIDO, CHIOMA WAYEYUKA Uk.14

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT BURUDANI TELE
JUMAMOSI APRILI 3, 2021



## WASANII WAJINADI

# Kwa Rais Samia Suluhu Hassan

Ni wazi awamu ya sita ya uongozi nchini Tanzania imeanza rasmi baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kukamilisha baraza lake la mawaziri.

Hatua hiyo imekuja baada ya aliyekuwa Rais Hayati Dk. John Magufuli, kufariki dunia Machi 17 na kuzikwa Machi 26 kijijini kwake Chato mkoani Geita.

Moja ya sekta ambayo ina matumaini makubwa katika uongozi wake ni sanaa. Baadhi ya wasanii tayari wametoa hisia zao kuhusu kiongozi huyo kwa kumwelezea kama mama mlezi, kiongozi makini na mwenye jicho la kuona mbali.

Mwanamuziki na mjasiriamali, Shilole, amesema ana imani na Rais Samia na ametangaza kuwa mfuasi wake rasmi kwa muda wote akiwa madarakani.

"Kuanzia sasa natangaza mimi ni mfuasi wa mama Samia Suluhu Hassan, wanawake tunaweza kufanya kila kitu nina imani kubwa naye," amesema Shilole.

Kwa upande wa mwigizaji Steven Nyerere, amesema kutokana na kasi anayoonyesha baada ya kuapishwa, anaweza kugombea tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

BASI SAWA

## Harmorapa amkumbuka Kiba



RAPA mwenye utata mwingi, Harmorapa, amesema alimwaga machozi baada ya kukutana na Alikiba kwa mara ya kwanza.

"Niliona kama ndoto kukutana na kaka Alikiba, dunia inamtambua kama mfalme wa muziki Africa, huyu jamaa ni mtu poa sana tofauti na watu wanavyomchukulia, ana nidhamu, heshima na upendo wa kweli kwa kila mmoja bila kubagua we niwa dizaini gani," amesema Harmorapa.

Amesema Ali kiba aliingia nyuma ya jukwaa sehemu yeye alikaa na wasanii wenzake, alipofika alimkumbatia na kufurahi sana kukutana naye.

Alikiba na Harmorapa walikutana siku ya mwisho ya kuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Pombe Magufuli huko wilayani Chato, mkoani Geita.

## Idris wakati mwingine unatulia


MSHINDI wa Big Brother Afrika na mchekeshaji, Idris Sultan, amewakabili wazazi kwa kuwaonya kuwa na uhakiki mzuri hasa kwenye masuala ya ndoa.

Idris Sultan amesema baadhi ya wazazi wanaogopa kuwaambia watoto wao kutoka kwenye ndoa kwa sababu ya maneno ya watu, wakati mtoto wao anakutana na matatizo.

"Ila wazazi kuna sehemu fulani inabidi mfanye mahojiano ya kina, unamshauri mwanao abaki kwenye ndoa ambayo anateseka, anateswa na mwenza wake, kimwili au kisaikolojia, ana msongo wa mawazo na hata majeraha mwilini, yote haya kisa wewe unaogopa maneno ya watu".

Ameandika.





## Wastara atoboa siri ya Rais Samia

MWIGIZAJI mkongwe nchini, Wastara Juma, amesema Watanzania wengi wanamuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa ana upendo wa dhati.

Amesema yeye ni mmoja wa watu walionufaika na upendo wake kwani alikuwa msaada kwake wakati anaumwa kwa kumpatia pesa za matibabu katika hospitali mbalimbali.

"Nakumbuka mwaka 2015 nilikuwa naye wakati wa kampeni, kule matatizo yalianza hadi nikaanguka jukwaani. Rais Samia alinishika mkono kwa kunisaidia gharama za matibabu na baadaye kusaidiwa na Hayati Rais John Magufuli," amesema.

## Dunia; Mwenye ngoma apige ipasuke

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA ni uwanja wa fujo, mwenye ngoma zake apige, acheze zipasuke. Ni msemo maarufu sana kwa watu wa pwani kama vile Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Mafia na Mombasa.

Maana ya msemo huu ni kumwacha mtu mwenye sifa, aendelee na sifa zake za kijinga, lakini mwisho wa siku ataumbuka.

Na hata mtu ambaye anadhulumu wenzake, ataambiwa hivyo, kwa maana kuwa ataendelea na tabia yake hiyo, lakini ipo siku itafika mwisho.

Filamu hii yenye mafunzo makubwa na ya kusikitisha imewashirikisha wasanii karibuni wote chipukizi na wenye uwezo mkubwa, wakiwamo watoto kama vile Star Mnoko, Rehema, Juma, Omas, Dizo, Sofia, Asha, Chris, Junior, Magora Luia na wengineo. Inaanza kwa kuwaonyesha watoto wawili, msichana na mvulana wenye umri kati ya miaka saba hadi 12 wakiwa wanaishi maisha ya tabu, dhiki na kila aina ya manyanyaso.

Hao ni Dizo na Rehema. Dizo ameamua kujipa hukumu ya kumtunza mdogo wake Rehema kwa kuacha shule na kufanya vibarua, ili dada yake asome.

Pamoja na kuishi maisha ya dhiki, lakini mtaani hapo watoto wao wananyanyapaliwa kwa madai wana maambukizo ya ugonjwa wa Ukimwi walioachiwa na wazazi wao ambao wamefariki dunia.

Watoto wa mtaani hapo wote wamekatazwa na wazazi wao kucheza nao, kwa sababu eti watawaambukiza.

Hata hivyo kwa kujiiba, watoto wamekuwa wakiwafuata na kucheza nao kwa sababu wanayoongea wazazi wao, hawayaelewi. Ndipo siku Dizo anapoawaeleza watoto wote walikwenda nyumbani kwao kwa siri, juu ya maisha yao.

Akawaambia si kweli kwamba yeye na dada yake wana ukimwi, ila aliyetengeneza stori ya uongo ni shangazi yao, ili aichukue nyumba ya urithi ya baba yao na wao kunyanyapaliwa.

Na ni yeye ndiye aliyemwongopea baba yao kuwa mama yao si mwaminifu na amepatwa na ukimwi.

Baba yao akamfukuza mama yao, lakini badala ya kuondoka akanywa sumu na baba yao alipoona hivyo akafa kwa presha.

Watoto kusikia hivyo wanaenda kuwasuta wazazi wao kuwa wamewaongopea. Kuna baadhi ya wazazi akili zikawarudia, wakaanza kutafuta ukweli kwa ushahidi na si kusikia tu.

Kumbe wakati Dizo anawasimulia ukweli jinsi ulivyo, kuna mtu mzima mmoja alisikia kila kitu.

Kwanza kabisa yeye alianza kwa kuwachukua watoto hao na kwenda kuishi kwake.





## Monalisa anena mazito

WASANII mbalimbali wamejitokeza kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kupata nafasi ya urais, na hivi karibuni mwigizaji Yvonne Cherrie maarufu Monalisa, aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram: "Wanawake wana uwezo wa kuongoza kama wanaume.

"Hatuwezi kuwa sawa na wanaume kimaumbile lakini tunaweza kuwa sawa nao kimawazo na mtazamo wa kiuongozi kujenga nchi," ameandika Monalisa.

Monalisa amesema kama watu wote wakiungana katika kumsaidia mama Samia, nchi itakuwa imara na itarithiwa na vizazi vijavyo ikiwa salama.




## Kwaheri Wanangu, Nenda Shujaa



**Na Adam Fungamwango**

BADO Watanzania tuko kwenye siku 21 za maombolezo ya msiba wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli. Alifariki dunia Machi 17 jijini Dar es Salaam na kuzikwa Chato mkoani Geita Machi 26.

Wanamuziki na wasanii bado wanamiminika studio kurekodi nyimbo za maombolezo, ambazo kwa sasa ndizo zinazopigwa kwenye televisheni na redio kwa ajili ya kuwaliwaza Watanzania kwenye msiba huu mzito.

Wiki iliyopita, tuliziangalia nyimbo za muziki wa dansi na bongo fleva ambazo 'zilitrendi' sana na kuwaliza watu kwenye msiba huo, kuanzia mwanzo kwenye kifo kilivyotangazwa, kuagwa na hata kuzikwa.

Leo pia tutaziangalia baadhi ya nyimbo 'zilizotrendi' kwenye maombolezo hayo. Lakini hizi sasa ni za 'gospel' na mahadhi mengine katofauti kabisa.

**Nenda Shujaa-Uinjilisti Kijitonyama Choir**

Kwaya ya Uinjilisti Kijitonyama imeliza sana watu kwa wimbo unaoitwa 'Nenda Shujaa'.

Ukiachilia mbali kuwa kwaya hii ni moja kati ya kwaya maarufu sana nchini kutokana na albamu zake nyingi kupendwa na kuuzwa kama njugu, pia ni wimbo ulioonekana ulirekodiwa mapema kabla ya msiba, lakini mazingira na maudhui ya wimbo huo yamefanana na msiba wenyewe, kiasi cha kuliza wengi kwenye msiba wa Dk. Magufuli.

Kwenye redio, televisheni, kwenye magari, na popote unapopita, wimbo huu imekuwa maarufu sana na kupendwa na wengi kutokana na jinsi ulivyotengenezwa, vyombo vyake na uimbaji, ukiakisi kile kilichotokea

"Nenda Shujaa nenda, maisha yako ni ushuhuda unaoishi..." Ni moja kati ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo wa huzuni.

**Kwaheri Wanangu-Varda Arts**

Hili ni kundi la zamani sana. Kwenye miaka ya 1980, lilitoa wimbo ulioitwa 'Maridadi Sana'. Halijafa. Bado Lipo. Ushuhuda ni kwamba kwenye msiba wa Dk. Magufuli limeingia studio na kutoa wimbo uitwao 'Kwaheri Wanangu'. Ni kama baba anayewaaga wanaye anapoenda safari ambayo hajui lini atarejea. Ni moja kati ya nyimbo za maombolezo zinazotia simanzi. Kama kawaida yao, wameuimba kiswahili, lakini kwenye mahadhi ya 'Kihindi'.

**Tanzania Twaiombea Amani-Wanawake WWC**

Hii ni kwaya ya wanawake Makao Makuu Dodoma. Kirefu inaitwa Warehouse Women of Christian Choir au WWC.

Ni kwaya ya wanawake watupu, ambao nao hawakuwa nyuma. Wakaingia studio na kutoa wimbo walioouita 'Tanzania Twaiombea Amani'. Ni wimbo maalum wa kuiombea nchi amani kutokana na janga lililoipata kuondokea na Rais ambaye bado alikuwa madarakani.


**Nenda Salama - Uvuke Choir**

Ni kwaya ya Kanisa ya Kianglikana Uvuke iliyopo Makao Makuu Dodoma, iliyotoa wimbo huu ulitwao 'Nenda Salama.'

Ni moja kati ya nyimbo bora kabisa za kwaya kwenye msiba huu wa kitaifa.

**Kwaheri Magufuli-Chuo cha Utumishi wa Umma**

Chuo cha Utumishi wa Umma nacho hakikuwa nyuma kutoa wimbo wa maombolezo. Ni miongozi mwa vikundi vya kwaya vilivyotoa nyimbo ambazo zimeleta faraja kwa Tanzania kwenye kipindi hiki kigumu.




# Maajabu 'kiatu cha shetani'

VIATU rangi nyeusi na nyekundu ambavyo vina picha ya shaba ya pentagram na msalaba uliogeuzwa huku ikinakshiwa kwa tone la damu halisi ya binadamu, vimeibua gumzo duniani kote.

Viatu hivyo vinavyojulikana kama 'Kiatu cha Shetani' kinaweza kuleta utata kwa dini zote, hasa baada ya kampuni inayotengeneza MSCHF kuweka sokoni pea 666 namba ambayo inaaminika ni ya kishetani.

Katika uzinduzi wake uliofanywa na rapa wa marekani, Lil Nas x, viatu vyote vilinunuliwa kwa kiasi cha dola za Marekani 1,018 kwa jozi pekee. Bei hiyo imelinganiwshwa na aya moja ya Biblia Luka 10:18 ambayo inasomeka: "Nilimwona Shetani akianguka kama umeme kutoka mbinguni."



## Mzee Edo awalaumu wanawake

MWIGIZAJI mkongwe wa Nollywood, Pete Edochie amelaumu wanawake kuwa chanzo cha kuongezeka kwa vurugu kwenye nyumba na ndoa kuvunjika.

Staa huyo wa sinema amesema vitendo vya unyanyasaji majumbani umekithiri kutokana na wanawake kukataa kufanya kile wanachotakiwa kama wake.

"Hiki kitu kinachoitwa usawa, ndicho kinachopelekea wanawake kupigwa kwenye ndoa. Unapozungumza na mwanamke, wakati anakujibu, hautaweza kuvumilia kwa hivyo utanyoosha mkono wako na kumpiga," amesema.

## Beyonce azidi kupata hofu

WASIWASI umezidi kutanda kwa familia ya mwanamuziki Beyonce baada ya watu kuvamia nyumba yake na kuondoka na mali za shilingi bilioni mbili.

Mtandao wa TMZ, uliripoti juzi kuwa watu hao walifanikiwa kuvamia nyumba hiyo ambayo Beyonce huwa anahifadhia mali zake ikiwamo vito vya thamani iliyopo mjini Los Angeles.

Kitu ambacho kinatoa hofu na kumuumiza kichwa Beyonce kuwa watu hao waliwezaje kuiba vitu hivyo tena kwa kurudia mara mbili bila kukamatwa na wala kujulikana na walinzi.





## Ringtone povu la nini?

MWIMBAJI wa Injili kutoka Kenya, Alex Apoko maarufu kama 'Ringtone' amekuja juu baada ya kuzushiwa madai ya ubakaji.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, aliweka video fupi ambayo akionekana akisema yote yanayozushiwa ni kwa sababu watu hawapendi maendeleo yake ya kimuziki.

"Acheni maneno yenu ya ovyo, mimi nitabaki kuwa juu, sipo hapa kwa sababu yenu, nipo hapa kwa sababu Mungu amewashinda akili nyinyi, hamuwezi kunishusha hata mkinizushia mabaya," amesema.

## Uchumba Davido, Chioma wayeyuka

FEBRUARI mwaka huu, mwanamuziki nyota wa Nigeria, Davido, alionekana akila bata na mwanamitindo Mya Yafai, wakati akiwa likizo katika visiwa vya carribian.

Baada ya tukio hilo, mjadala mkali ukatanda katika mitandao ya kijamii kuhusu penzi la msanii huyo na mchumba wake Chioma kama lipo hai au limevunjika.

Hata hivyo, Jumanne ya wiki hii Davido aliachilia picha nyingine akiwa na mrembo huyo mpya na hapo ndipo ilipodhihirika kuwa imekuwa mwisho wa 'kapo' hiyo iliyowavutia wengi nchini humo.



# JPM ameacha ujumbe mzito kwa Watanzania

Na Dk. Enock Mlyuka

KUZALIWA ni bahati, bali kufa ni lazima. Kifo ni fumbo la maisha. Mtu anaweza kujua alikotoka, mahali alipo sasa, lakini yajayo mbele yake hayajui.

Ukweli huu umethibitishwa zaidi na kifo cha Dk. John Magufuli, aliyekuwa Rais wa Tanzania. Magufuli alikuwa zawadi ya Watanzania, mwanga na dira ya maendeleo ya Tanzania. Kifo chake kimejeruhi na kuumiza nafsi za Watanzania na kuleta simanzi kubwa.

Kifo chake kimekuwa cha ghafla kwa Watanzania kwa kuwa hakuna mtu aliyewahi kuwaza kama angefariki dunia katika kipindi ambacho Watanzania walikuwa bado wanamhitaji. Kwa kifo chake, Tanzania bado inahitaji rehema na faraja ya Mungu.

Vilio na machozi ya watu wengi juu ya kifo cha Magufuli ni dhahiri kuwa utumishi wake ulipokewa na kukubalika na watu wengi ndani na nje ya Tanzania. Umati mkubwa wa kihistoria uliojitokeza kumuaga ni uthibitisho tosha kuwa alikuwa chaguo sahihi na halali la Watanzania.

Utumishi wake umeacha alama na ujumbe kwa Taifa la Tanzania na dunia. Utumishi wa Magufuli umegusa maisha na mioyo ya Watanzania wengi, hasa watu wa hali ya chini. Aliyatoa maisha yake kuwa sadaka kwa nchi yake na watu wake. Alikuwa mpambanaji na kipenzi cha Watanzania wengi.

Alitetea taifa lake kwa ujasiri na msimamo usioyumba, hali ambayo iliwafanya Watanzania wajiamini. Magufuli hakuwa kiongozi tu, bali alikuwa kuhani aliyetegemeza watu wake katika Mungu na alitambua kwamba hakuna maendeleo pasipo mkono wa Mungu.

Magufuli alileta tumaini jipya katikati ya mahangaiko. Alitanguliza maslahi ya taifa kuliko maslahi binafsi akitambua kuwa faida binafsi haijengi bali huumiza taifa. Magufuli atakumbukwa kwa mazuri mengi na mapenzi yake ya dhati kwa nchi yake na watu wake.

Thamani ya mtu haipimwi kwa wingi wa siku za kuishi kwake, bali kwa matendo yake wakati wa uhai wake. Magufuli ataendelea kuishi katika mioyo ya Watanzania kutokana na mema mengi aliyolifanyia taifa wakati wa uhai wake. Ameondoka akiwa ameiacha Tanzania yenye heshima na inayokua kwa kasi kiuchumi.

Hakika amefanya kazi kubwa inayostahili thawabu mbele za Mungu na wanadamu. Magufuli ameonyesha njia na kuwafumbua macho Watanzania. Ameachia ujumbe mzito katika uongozi, utawala, na usimamizi thabiti wa rasilimali za nchi.

Pamoja na mambo mengine mengi, Magufuli amefundisha uadilifu na kupenda kazi, kujiamini na kujithamini, kuwajibika, kuwa na msimamo, kukataa tabia ya unafiki, kujali wanyonge kwa kuwa ziko baraka za Mungu kwa kufanya hivo. Amewafundisha Watanzania uzalendo na kupenda vya kwetu ili kuondokana na aibu ya kunyonywa na mabeberu. Historia yake itaendelea kujiandika, hivyo jukumu kubwa la Watanzania ni kuzikumbuka kazi zake na kumuenzi kwa vitendo.



Daraja la Juu la Kijazi lililoko Ubungo, Dar es Salaam, ambalo ni moja ya alama alizoziacha Hayati Magufuli. **PICHA: MAKTABA.**

Magufuli hakuongoza nchi kama malaika, bali aliongoza kama mwanadamu anayeweza kukosea kwa kuwa kukosea ni kwa kila binadamu. Kwa hiyo, binadamu mwenye akili timamu, aliyekomaa kifikra na anayejitambua, ataangalia zaidi mema ya Magufuli na kuyaenzi kuliko kuangalia upungufu wake. Amekamilisha kazi aliyotumwa kuifanya akiwa hai, hivyo inatakiwa kuendelezwa kuanzia alipoishia.

Huu si wajibu wa Rais Samia Suluhu Hassan peke yake, bali ni wajibu wa kila kiongozi na kila Mtanzania mahali alipo. Kila mmoja akitimiza wajibu wake kwa uaminifu, Tanzania itakua kiuchumi na ustawi wa jamii kama ilivyokuwa ndoto na maono ya Magufuli.

Ni neema ya Mungu kwamba Mungu amewapa Watanzania Samia kuwa Rais wa sita wa Tanzania na mwanamke wa kwanza nchini kuwa Mkuu wa Nchi na Amiri Jeshi Mkuu. Pia ni mwanamke wa sita katika Bara la Afrika kushika wadhifa wa urais katika nchi.

Yote haya ni mapenzi yake Mungu na historia imeandikwa Tanzania. Mama huyu ni kiongozi aliyepikwa na kuiva. Uzoefu, uwezo na chuo cha Magufuli alichopitia si mambo ya kupuuzwa. Magufuli alimwandaa bila kujua anamwandaa na Samia aliandaliwa bila kujua kuwa anaandaliwa kwa wajibu mkubwa wa kuliongoza taifa.

Uongozi ni haki ya kila mwenye uwezo. Huu ni wakati wa Samia kuendelea kuthibitisha kuwa wanawake wanaweza wakipewa fursa na nafasi za uongozi kwa kuwa Mungu amewekeza nguvu ya mabadiliko na vipawa vingi ndani ya wanawake.

Wajibu wa Watanzania ni kumpa ushirikiano na kumwombea ili aongoze kwa hekima, upendo na katika msimamo. Watanzania wasiogope wala kufadhaika. Waendelee kumwomba Mungu ili ailinde nchi na maadui na wote wenye jicho la husuda!

**Mungu ibariki Tanzania! Mungu ibariki Afrika.**

**[Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maoni, mafunzo na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au WhatsApp +255655865555.]**



Hayati Rais Magufuli.

# NMB yamuenzi Dk. John Magufuli kumwinua kifedha 'Mwanamke Jasiri'

**Na Moshi Lusonzo**

TANZANIA bado ipo katika kipindi cha maombolezi ya siku 21, baada ya aliyekuwa Rais wa awamu ya tano Dk. John Pombe Magufuli kufariki dunia Machi 17, mwaka huu.

Kulingana na matakwa ya kikatiba, aliyekuwa makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, aliapishwa na kuwa kiongozi mkuu wa nchi.

Katika kipindi hicho kigumu watu binafsi, taasisi za kiserikali na zile binafsi, zinaendelea kuenzi kazi nzuri zilizofanywa na Hayati Rais Dk. Magufuli, pia kumpongeza na kutarajia mambo mazuri kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Benki ya NMB ni moja ya taasisi ambayo inamuenzi Dk. Magufuli kwa njia tofauti, nayo ni kuanzisha mpango maalum wa kuwawezesha wanawake kuingia katika ujasiriamali ili kujiinua kiuchumi.

Kati ya mambo makubwa yaliyofanywa na Benki ya NMB mwaka 2020 na itaendelea kufanya ni kuzindua klabu maalumu kwa ajili ya wanawake nchini inayoitwa 'Mwanamke Jasiri'.




Mgeni rasmi katika hafla ya uzinduzi wa 'NMB Women's Club Networking' Jaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania, Joaquine De Mello), akizungumza alipokuwa akizindua jukwaa hilo lililopewa jina la NMB Mwanamke Jasiri lililozinduliwa na Benki ya NMB, jijini Dar es Salaam.




Jaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania, Joaquine De Mello (wapili kushoto) na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Benki ya NMB, Juma Kimori (katikati) na Ofisa Mkuu wa Huduma Jumuishi wa Benki ya NMB, Nenyuata Mejooli (kulia), wakionyesha vipeperushi vya NMB Mwanamke Jasiri ikiwa ni ishara baada ya kuzindua jukwaa hilo, jana.

Mwanamke Jasiri ni mkusanyiko wa bidhaa na huduma mbalimbali zinazoweza kumsaidia mwanamke kiuchumi na kuwainua kibiashara na kuwaonyesha fursa wanazoweza kuzipata kupitia benki hiyo.

Ndani ya kifurushi cha 'Mwanamke Jasiri' kuna Fanikiwa Akaunti, Pamoja Akaunti, Mikopo ya wanawake waajiriwa, NMB Mkononi, NMB Bima na Dunduliza na NHIF.

Ofisa Mkuu wa Huduma Jumuishi wa NMB, Nenyuata Mejooli, anasema lengo la huduma hiyo mpya si tu kuwawezesha wanawake wa Kitanzania kiuchumi, bali kuwaimarisha kibiashara na kuwajengea uchumi wao ili waweze kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa.

Anasema kwa mujibu wa Financial Alliance for Women, ambayo ni muungano wa taasisi za kifedha za kimataifa zenye mlengo wa kumkwamua mwanamke kiuchumi, NMB inaongoza kuwapa kipaumbele wanawake katika huduma zake.

Muungano huo ulioanzishwa mwaka 2000, unaiona benki hiyo ina rekodi ya kipekee nchini na katika ukanda wa Afrika Mashariki katika masuala ya kuwaelimisha wanawake kuhusu masuala ya kifedha na kuwakutanisha kwa ajili ya kuwapa mafunzo mbalimbali.

Takwimu zilizopo kwenye tovuti yake zinaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 47 ya wafanyakazi wa benki hiyo ni wanawake.

Taasisi hiyo ya Financial Alliance for Women, yenye makao yake makuu jijini New York, Marekani, inasema takribani asilimia 30 ya wateja wa benki hiyo kuwa wanawake ambao wanapata karibu asilimia 31 ya mikopo.

Baada ya uzinduzi wa programu ya Mwanamke JASIRI, NMB iliwakutanisha wajasiriamali wanawake na wafanyabiashara zaidi ya 170 katika mdahalo wenye mada zilizokuwa chachu ya ushiriki wao katika huduma rasmi za kifedha.

"Kwa utaratibu huu mpya wa huduma wa NMB, elimu, mafunzo na kutukutanisha... wanawake tutaweza sana na zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali... Hii ni zaidi ya mwanamke akiwezeshwa anaweza," mmoja wa washiriki, Mercy Robert wa Mbezi Louis, aliliambia gazeti hili.

Jaji wa Mahakama ya Rufani, Joaquine De Mello, ameipongeza Benki ya NMB kwa kung'amua uwezo na nguvu za wanawake katika maendeleo na kujikita kuwasaidia.

Anasema benki hiyo kuamini wanawake kuwa kitu kimoja, wakajua fursa zilizomo ndani ya NMB kama vile mikopo na elimu ya biashara ni jambo jema litakalowasaidia kutumia fursa zilizopo kwa ajili ya maendeleo yao binafsi.

Jaji De Melo alifafanua kuwa katika muktadha huo, wanawake wa Kitanzania watawezeshwa kutoa mchango stahiki na mwisho kulikomboa taifa kiuchumi.

Mwanasheria huyo anaeleza pamoja na wanawake kuwa wengi kitakwimu na wazalishaji wakubwa, bado ushiriki wao katika huduma rasmi za kifedha ni mdogo na usiokuwa na tija kubwa kimaendeleo.

"Sina tafiti binafsi lakini najua kuna changamoto mbalimbali zinazosababisha mkwamo huo ikijumuisha uelewa wa mbinu na stadi za biashara, ujasiri na kujiamini ni baadhi tu ya changamoto hizo," anaongeza Jaji De Mello.

Anasisitiza kwa kusema "Nawapongeze NMB kwa kulibeba hili na kuandaa programu maalumu ya uwezeshaji, uhamasishaji na elimu, ili nasi wanawake tufaidike katika huduma za kibenki hususani kukopa."

Kwa mujibu wa Benki ya Dunia, asilimia 79 ya wanawake nchini walikuwa sehemu ya nguvu kazi kufikia mwaka 2017 lakini ni asilimia 19 tu ndio waliokuwa na akaunti katika taasisi rasmi ya kifedha.

Kwenye uwekaji akiba, takwimu kutoka Global Findex zinaeleza kuwa hilo linafanyika katika taasisi rasmi kwa asilimia nne tu huku ukopaji ukiwa asilimia tano pekee.

Madhumuni ya mpango wa Mwanamke Jasiri ni kusaidia kurekebisha kasoro hizo na nyingine nyingi zinazowakwamisha wanawake kimaendeleo kwa kuwakwamua kiuchumi na kuwaimarisha kibiashara.

Nenyuata anasema NMB imejipanga vizuri kulipatia ufumbuzi tatizo hilo kwa kutoa huduma nzuri za kibenki, zenye tija na zinazoendana na mahitaji ya wanawake nchini.

Anaeleza kuwa benki hiyo inaamini wanawake wakiwa kitu kimoja, wakajua fursa zilizomo kama vile mikopo na elimu ya biashara; wanaweza kutumia kwa maendeleo binafsi, familia zao na taifa kwa ujumla.

Mjasiriamali ambaye anamiliki duka la nguo la Wedding Lydia, Lydia Monyo, anaeleza aafari yake ilianza miaka 10 iliyopita akiwa kama mfanyabiashara mdogo mpaka sasa amekuwa na mtaji mkubwa.

"Wameweza kunihudumia na kunipatia mtu wa karibu wa kunihudumia pindi ninapopata changamoto za biashara. Nawashauri wafanyabiashara wadogo wadogo na wakubwa pia wasisite kuitumia Benki ya NMB."

HABARI KIMATAIFA

# Mashua kutoka Palma yawasili Pemba Msumbiji

**Cabo Delgado,** MSUMBIJI

MASHUA iliyowabeba waathirika wa mashambulizi yanayoendelea katika mji wa Palma, iliwasili salama katika mji mwingine nchini Msumbiji.

Manusura 1,200 waliosham-buliwa na wanamgambo wa Ki-islam Kaskazini mwa nchi hiyo katika jimbo la Cabo Delgado, waliwasili katika Bandari ya Pemba, juzi jioni.

Wahudumu wa kutoa misaada walikuwa katika bandari hiyo kuwapa manusura hao chakula huku polisi na wanajeshi waki-dhibiti hali hiyo hasa kutokana na hisia nzito za jamaa kuungana na wapendwa wao waliookole-wa wakati wa mashambulizi hayo yaliyoanza wiki iliyopita katika eneo la Palma.

Zaidi ya watu 8,000 walilazi-mika kuyakimbia makazi yao, baada ya watu kadhaa kuuawa kwa kukatwa vichwa na nyumba zao kuchomwa moto.

Watu wengi bado hawaju-likani waliko baada ya masham-bulizi hayo ya Machi 24, ambako wahudumu wa kutoa misaada walisema wengi wa watu hao wanaaminika kukimbilia misi-tuni au kutoroka kutumia boti.

Watu wanaoshukiwa kuwa wanamgambo wenye itikadi kali za kidini wamekuwa wakifanya mashambulizi katika mkoa wa Cabo Delgado wenye utajiri mkubwa wa mafuta na gesi asilia tangu Oktoba 2017.

**DW**



Kiongozi wa Kanisa la Katoliki Duniani, Papa Francis akiendesha misa usiku wa kuamkia jana Ijumaa Kuu katika Kanisa Kuu la Mt. Peter Balisica, Vatican. **(PICHA: AFP)**

# Ajali ya treni yaua 48 Taiwan

**Hualien, TAIWAN**

TRENI ya abiria ikiwa na abiria takribani 500 imepata ajali ka-tika handaki na kuua watu 48 na kujeruhi wengine 66.

Picha kutoka eneo la tukio zilionyesha waokoaji wakiwaon-doa manusura kwenye ajali hiyo.

"Watu waliangukiana na ku-kanyagana," alisema mmoja wa wanawake aliyenusurika.

Ajali hiyo ilitokea Kaskazini Mashariki mwa mji wa Hualien, na dereva wa treni ni kati ya waliofariki.

Pia treni hiyo ilikuwa imebeba watalii ambao walikuwa wakire-jea nyumbani kuanzia likizo ya wiki ya sikukuu.

Taarifa zilisema treni hiyo ili-kuwa ikitoka, Taipei, mji mkuu uliopo Kusini Mashariki mwa Taitung.

Waziri wa Uchukuzi, Lin Chia-lung aliwaambia waandishi wa habari, kwamba treni ilibeba abiria 490 idadi ambayo ni kub-wa kuliko iliyotakiwa 350.

Pia ilielezwa treni hiyo il-iteleza na kupoteza mwelekeo na kwamba idadi kubwa ya abiria walikuwa wamesimama kwenye treni.

**REUTERS**

## Misri yatafuta dola bilioni 1 kufidia hasara Suez

**Cairo,** MISRI

MAMLAKA ya Mfereji wa Suez ya Misri (SCA) imesema, inatafuta zaidi ya dola bilioni moja za Kima-rekani kufidia ya hasara iliyosaba-bishwa na meli ya makontena ya Ever Given.

Meli hiyo ilikwama kwenye njia ya maji na kuzuia usafirishaji kwa siku sita, Mwenyekiti wa SCA, Osama Rabie, alisema.

"Itagharimu hasara za tukio hilo, itafikia bilioni moja," Rabie aliiam-bia televisheni moja.

Meli hiyo iliyobeba tani 224,000 ilikwama Machi 23, mwaka huu, na ilitolewa na SCA kwa kushirikiana na kampuni ya Uholanzi.

Meli zote 422 zilizocheleweshwa zitakuwa zimevuka Mfereji wa Suez, kulingana na Rabie.

Asilimia 12 ya biashara duniani hupitia mfereji uliotengenezwa na binadamu.

**XINHUA**

## Papa aongoza misa Ijumaa Kuu

**Vatican City,** ITALIA

WAKATI wakristo wakiadhimisha siku ya Ijumaa Kuu, jana, kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis aliiadhimisha siku hiyo akiwa chini ya vikwazo vikali ku-fuatia janga la virusi vya corona.

Papa Francis aliadhimisha kum-bukumbu ya kuteswa kwa Yesu Kristu katika ibada iliyofanyika kwenye Kanisa la Mtakatifu Petro wa Basilica.

Kulingana na Vatican ni waumini wachache tu waliruhusiwa kuhud-huria ibada za Papa katika sikukuu za Pasaka kwa sababu ya hatua za kuzuwia kusambaa kwa virusi vya corona.

Kama ilivyokuwa mwaka jana pia mwaka huu hakukuwa na ibada ya njia ya Msalaba ambayo kwa kawaida hufanyika katika eneo la Colosseum katikati ya jiji la Rome.

Na badala yake kulifanyika ibada ndogo za njia ya Msalaba katika bustani ya Mtakatifu Petro mbele ya Kanisa la Basilica.

**BBC**

# MATUKIO IBADA YA IJUMAA KUU





Waumini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania Usharika wa Arusha Road, jijini Dodoma wakishiriki ibada ya Ijumaa Kuu jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Askofu wa Kanisa la Angalikan Dayosisi ya Central Tanganyika, Dk. Diksoni Chilongani akisalimiana na Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, baada ya kumalizika kwa ibada ya Ijumaa Kuu, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**



Waumini wakimsikiliza Paroko wa Kanisa la Katoliki Parokia ya Yohana Maria Muzeey Tegeta A, wakati wa ibada ya Ijumaa Kuu katika Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Dodoma, Amoni Kinyunyu, akitoa mahubiri kwenye ibada ya Ijumaa Kuu katika Usharika wa Arusha Road, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Waumini wa KKKT Usharika wa Azania Front, wakiigiza mateso ya Yesu Kristo, wakati wa ibada ya Ijumaa Kuu, jijiji Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**HADITHI**

MAUAJI ya kutisha yanatokea ndani ya gesti moja maeneo ya Kigogo jijini Dar es Salaam. Mfanyabiashara Burhan anauawa ndani ya gesti ya Tukutane, akiwa na msichana mmoja mrembo aitwaye Mwanaidi. Polisi wanawakamata watu wote waliokutwa humo, pamoja na wafanyakazi wa gesti hiyo kwa ajili ya mahojiano. Lakini inaonekana muda ambao walikuwapo wapenzi hao hakukuwa na mteja mwingine yeyote zaidi yao. Baada ya mahojiano ya kina, inaonekana kabisa kuwa Mwanaidi ndiyo muuaji. Je, ni kweli? Kwa nini alimuua mpenzi wake wakiwa wamejifungia chumbani? Fuatilia hadithi hii kwa makini ambayo mbali na kukutia simanzi, furaha na kukuburudisha, pia itakufundisha, elimu na kufunulia mambo ambayo hukupata kuyafikiria kabla.

# Lazima Apatikane-**15**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

“Kwanza kabisa nilianza kuwa na wasiwasi juu wa msichana kama Mwanaidi, ambaye ana miaka 25 tu nadhani kuwa na uwezo wa kushika kisu na kumuua mtu kama Burhan kwa kumchoma mara nne kifuani kwa uzito ule ule, kwani niligundua kuwa muuaji alitumia nguvu kubwa kudidimiza kisu mwilini. Kwa mwanamke wa kawaida, ambaye hana historia ya ujambazi au kuua, inakuwa si rahisi.” Akasema na kuwafanya wenzake kuanza kupata somo ambalo hawakulijua kabla.

“Eti amemuua kisa tu ni milioni 100 zilizokuwa kwenye kifuko, lakini tukumbuke kuwa Burhan ni jambazi katili na mzoefu, isingewezekana mtu kama huyo kufanya kazi kubwa ya kupora, kuua wenzake watatu, halafu akaenda na mwanamke gesti, akakaa kizembezembe au kupitiwa na usingizi hadi kuchomwa kisu mara nne kirahisi vile. Nilianza kuhusi kuwa aliyemchoma kisu Burhan huenda naye alikuwa na uwezo na akili kama yeye. Hilo lilinifanya nianze kufikiri namna ya kutafuta namna nyingine ya kumtafuta mtu mwingine ambaye anaweza kuwa muuaji. Msichana kama Mwanaidi hata kama Burhan angelala usingizi, sidhani kama angemchoma kisu mara nne kwa nguvu ile ile bila woga wowote.”

Koplo Hamisi na Inspekta Msiya walitazamana na kutikisa kichwa. Waliona kuwa kulikuwa na vitu fulani vvya ndani ambavyo wao hawakuvitambua kabla.

“Ndiyo maana niliomba msichana huyu apewe dhamana. Nilijua yeyote ambaye yupo nyuma ya mpango huu atakuwa anamfuatilia. Na lengo lake ni kwamba Mwanaidi anyongwe au afungwe maisha ili yeye awe salama. Na kama ataachiwa, basi mtu huyo atamtafuta ili ammalize kwa ajili ya kupoteza ushahidi.” Alinyanyua kikombe cha kahawa, akapiga mafunda kadhaa na kuweka mezani.

Wakati huo Mwanaidi ambaye alikuwa amekuja naye asubuhi kuripoti, yupo kwenye ofisi nyingine ya upelelezi. Yeye hakuwa kwenye kikao hicho kwa sababu hakimhusu.




“Kingine kikubwa zaidi kuwa dunia ya sasa ni ya teknolojia. Nilijua mtuhumiwa kama akiachiwa angekuwa kwenye hatari kubwa, hivyo nilimpa kifaa cha kisasa ambacho kinarekodi mwenendo wa mtu au kitu popote kilipo au kinapokwenda ‘Global Positioning System’, au maarufu kama ‘GPS’. Baada ya mkutano ule na mlipokubali atoke kwa dhamana, nilikutana naye na nikampa kifaa hicho na maelezo jinsi ya kufanya. Nikamwambia muda wote awe na kifaa hicho na mimi nitakuwa namfuatilia. Hiki kifaa alikiweka kwenye nywele zake na mimi nilikuwa najua yupo wapi, ana kwenda wapi na kilichukuwa kinachokua picha na hata sauti. Kwa hiyo maafande wenzangu, hata alipokwenda kuchukuliwa na yule jambazi Martin na kumpeleka ofisini mwake na lengo la kumlazimisha kumuua Tika, mimi nilikuwa nafuatilia kila kitu.”

Akasema huku akikumbuka pia usiku wa jana akiupitisha akiwa na Mwanaidi nyumbani kwake Mburahati, Dar es Salaam.

“Ndiyo maana haikuwa ngumu kwangu mimi kwenda Kifuma Bar kutibua mpango wake wa kumlazimisha Mwanaidi amuue Tika, lakini kumlinda kwani nilijua kitendo cha Martin kujua Tika hajafa, basi angemuua msichana huyu. Pia nilianza kuwa wasiwasi kuwa huenda anaweza kuwa ndiye muuaji wa Burhan.”

Aliinua tena kikombe cha kahawa akanywa yote iliyobaki. Akaweka kikombe kitupu chini na kuendelea.

“Nilikafanya mpango ule na jamaa wa kaunta akabadilisha kifuko, akatoa kile chenye sumu halisi na kukiweka nilichompa baada ya kukagua, baada ya hapo nikawahi nyumbani kwa msichana nikasikia mazungumzo yote ya Martin akijinasibu kuwa yeye ndiye muuaji, nikarekodi na flashi yake ndiyo hii hapa ambayo mmeisikiliza”

**Koplo Hamisi na Inspekta Msiya walitazamana na kutikisa kichwa. Waliona kuwa kulikuwa na vitu fulani vvya ndani ambavyo wao hawakuvitambua kabla.**

Kila mtu ndani alishangazwa na weledi mkubwa na ujanja wa hali ya juu wa Jan alioutumia kumkamata muuaji.

“Kingine ni kwamba isingewezekana na msichana kama huyu eti kuchukua mfuko wa pesa wa mamilioni ya shilingi, akaenda kuuficha na kurudi tena eneo la tukio, akajifanya amezirai. Niliunganisha viulizo vyote hivyo nikaona huenda kuna mtu nyuma ya pazia ambaye sisi hatumjui anafanya kazi hii. Tena ni mzoefu, kwani anafanya kazi kwa ufanisi bila kuacha alama au ushahidi. Ninavyojua angekuwa huyu msichana kama angechukua pesa asingerejea tena. Hapo nitajua kuna mtu mwingine ambaye ni jambazi sugu kama Burhan mwenyewe aliingia. Akamuua na kuchukua pesa, akaondoka nazo. Hapo ndipo nilipoandaa huo mkakati.”

Baada ya kumaliza, wakubwa wake wanampongeza na kuahidi kumpandisha cheo kutokana na kazi kubwa.

Pia wakaamuru jadala ya kesi ya mauaji lililokuwa linatakiwa kwenda mahakamani iondolewe na sasa awe huru.

*******************************

“Usiniambie Jan?”

“Basi sikwambii.”

“Hebu rudia tena?

“Uko huru Mwanaidi. Muuaji halisi amepatikana. Siyo wewe.”

“Waooo siamini. Najua muuaji siyo mimi, ila dunia nzima ilidhani ni mimi. Ni wewe pekee umepambana hadi kumjua muuaji. Tena kwa ushahidi kamili. Nashukuru sana. Sijui nikupe zawadi gani?” Mwanaidi alimkumbatia Jan, wakiwa wanatoka kwenye ofisi za Makao Makuu ya Polisi.

“Hii ni kazi yangu ya kutumikia wananchi Mwanaidi. Sihitaji zawadi.” Akasema Jan, wakiwa tayari wameshatoka eneo la Makao Makuu ya Polisi.

“Sasa tunaenda wapi?” Mwanaidi akamuuliza.

“Mimi naenda nyumbani.”

“Na mimi naenda huko huko.”

“Kwangu?” Jan aliuliza.

“Ndiyo, jana si ulilala kwangu, leo kwako. Si ulisema huna mke?”

Jan alimtazama Mwanaidi. Alikumbuka jinsi alivyoupitisha usiku jana kuamkia leo akiwa nyumbani kwake.

Akajikuta akimpapasa nywele zake ndefu na kujibu.

“Haya, kwa unavyotaka wewe. Sina neno. Twende.” Jibu hilo lilimfanya Mwanaidi amtazame kwa bashasha na tabasamu la aibu za kike.

**MWISHO**

# MBAPPE: NITAZUNGUMZA AKILI YANGU IKITULIA



**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe amesema hakuna chochote kinachoendelea juu ya yeye kusaini mkataba mpya na Paris Saint-Germain, huku uvumi ukimhusisha kuihama klabu hiyo kipindi cha majira ya joto mwaka huu.

Nyota huyo wa PSG amekuwa akihusishwa na Real Mdrid pamoja na Barcelona huku Liverpool nayo ikionyesha nia ya kuisaka saini ya nyota huyo ambaye mkataba wake unatarajiwa kumalizika mwakani.

Mbappe amesema kwa sasa hana taarifa yoyote kama atasaini mkataba mpya na miamba hiyo ya Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, na hivyo ataendelea kukaa kimya hadi mazungumzo yatakapofanyika.

Akizungumza na RTL baada ya Ufaransa kushinda 1-0 dhidi ya Bosnia-Herzegovina kwenye mchezo wa kufuzu Kombe la Dunia 2022, Mbappe alisema kwa sasa hana cha kuzungumza kuhusu mkataba mpya na PSG.

"Kama ningekamilisha mazungumzo ningezungumzia jambo hili, na nitazungumza pale akili yangu itakapotulia," alisema Mbappe.

Mbappe alisajiliwa kwa dau kubwa na PSG la pauni milioni 125 wakati akitoka Monaco mwaka 2017.

# Chelsea nayo yajitosa kumwania Wijnaldum

**LONDON,** England

CHELSEA imeingia katika kinyang'anyiro cha kuwania saini ya Georginio Wijnaldum ambaye yupo kwenye mipango ya kutua Barcelona mwishoni mwa msimu huu.

Kiungo huyo wa Liverpool amehakikishiwa kuungana na Kocha, Ronald Koeman ambaye ni raia mwenzake wa Uholanzi pale Camp Nou, mara tu mkataba wake utakapofikia mwisho.

Kocha, Jurgen Klopp alikuwa akiamini atambakisha Wijnaldum, lakini mazungumzo yameshindikana kati ya mchezaji huyo na klabu.

Na iliripotiwa kwamba, uhamisho wa Wijnaldum wa kwenda Barcelona ulikuwa umefanyika kwa asilimia 95, baada ya kumkosa msimu uliopita.

Lakini gazeti la Marca limeandika jinsi klabu hiyo ya Ligi Kuu England ilivyojiunga kwenye orodha ya klabu zinazowania saini ya mchezaji huyo pamoja na Juventus na Paris Saint-Germain.

Usajili wa kipindi cha majira ya joto utampa fursa kocha wa sasa wa Chelsea, Thomas Tuchel kufanya usajili wake wa kwanza baada ya kuchukua mikoba ya Frank Lampard aliyetimuliwa Januari mwaka huu.

Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30 anajiandaa kuondoka Liverpool baada ya kuitumikia klabu hiyo kwa kipindi cha miaka mitano.

Alifanikiwa kunyanyua taji la Ligi Kuu England msimu uliopita baada na pia amebeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Klabu Bingwa ya Dunia.







# Sergio Ramos kuikosa Liverpool, El Clasico

**MADRID,** Hispania

NAHODHA wa Real Madrid, Sergio Ramos, atazikosa mechi zote mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya robo fainali dhidi ya Liverpool baada ya kuumia nyama za kigimbi.

Mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 35 aliumia wakati akiwa kwenye majukumu ya Timu ya Taifa.

Madrid itacheza na wekundu hao wa Anfield Jumanne ya Aprili 6, mwaka huu na mchezo wa marudiano utapigwa Jumatano ya Aprili 14, mwaka huu.

Huku pia Aprili 10, mwaka huu timu hiyo itavaana na Barcelona kwenye mchezo wa El Clasico wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

"Kama kuna kitu kinaniuma basi ni kushindwa kuisaidia timu yangu kwenye mechi hizi muhimu," aliandika nahodha huyo wa Hispania kupitia ukurasa wake wa Instagram.

Ramos amesema aligundua tatizo lake hilo wakati akiwa kwenye mazoezi baada ya Hispania kushinda mabao 3-1 dhidi ya Kosovo na akafanyiwa vipimo Alhamisi na kuthibitika kwa majeruhi hayo.

Real Madrid itaanzia nyumbani kwenye mchezo wake wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool.

Mchezo huo ulikuwa unasubiriwa kwa shauku kubwa na mashabiki baada ya Ramos kumuumiza fowadi Mohamed Salah, ambaye aliumia bega kwenye fainali ya mwaka 2018 ya michuano hiyo jijini Kiev nchini Ukraine.

HABARI MICHEZO

# Ronaldo aomba radhi wanawake

**MADRID,** Hispania

GWIJI wa soka wa Brazil, Ronaldo Luis Nazario de Lima ameomba radhi kwa staili yake ya nywele aliyotaja kuwa ya ovyo sana, aliyonyoa kwenye fainali za Kombe la Dunia mwaka 2002.

Ronaldo amesema anawaomba msamaha kinamama wote duniani ambao watoto wao waliiga mtindo huo wa kunyoa nywele.

Straika huyo alinyoa kipara kote na kubakiza pembe tatu juu ya paji la uso, mtindo ambao mwenyewe alidai alibuni ili kuwafanya watu kusahau kwamba yeye ni majeruhi na kuzungumzia nywele zake.

Ronaldo mwenye umri wa miaka 44, ambaye kwa sasa ni rais wa klabu ya Valladolid inayocheza Ligi Kuu Hispania, LaLiga, ameelezea staili yake hiyo ya nywele kuwa ya ovyo sana katika mahojiano na Sports Illustrated.

Ronaldo alisema: "Nawaomba radhi kinamama wote ambao watoto wao waliiga kwa kukata nywele zao mtindo nilionyoa.

"Niliponyoa staili ile, wachezaji wenzangu waliniuliza, 'Umeipenda?' Walisema, 'Hapana, ni ya ovyo! Nyoa nywele zote!' Lakini, waandishi wa habari waliona staili ya nywele na kusahau habari za majeruhi."

Ronaldo, anahesabika kama mmoja wa mastraika bora kabisa kwenye historia ya soka na alisema jina lake amepewa baada ya daktari aliyemzalisha mama yake katika hospitali moja huko Rio de Janeiro.

"Daktari alimzalisha mama yangu bure kwa sababu wazazi wangu hawakuwa na uwezo wa kulipia gharama.






# VARANE AJIANDAA KUTIMKA MADRID

**MADRID,** Hispania

MTANDAO wa Newsnow wa nchini Uingereza umeripoti kuwa beki wa Real Madrid, Raphael Varane ana mpango wa kuondoka hapo kwenye dimba la Santiago Bernabeu mwishoni mwa msimu huu.

Varane ameripotiwa kuwa kwenye rada za Manchester United ambayo inamfukuzia kwa udi na uvumba kumnasa raia huyo wa Ufaransa.

Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer yupo katika mikakati wa kusajili beki mpya wa kati klabuni hapo atakayecheza na Harry Maguire.

Victor Lindelof na Eric Bailly ndio mara nyingi huwa wanacheza na nahodha huyo, lakini hawajamshawishi Solskjaer kuwa ndio watakuwa suluhisho la muda mrefu la nafasi hiyo.

Mchezaji huyo atabakiza miezi 12 pindi dirisha la usajili litakapofunguliwa ndio maana 'Le Blancos' hawataki kuweka vikwazo vingi kwa timu inayomtaka ili asiondoke bure.

# Pogba rasmi kuondoka United

**MANCHESTER,** England

NI wazi sasa kiungo wa Manchester United, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28 ataondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu.

Gazeti la Daily Mail limeripotiwa kwamba, Pogba anaondoka klabu hapo akielekea kwa waajiri wake wa zamani Juventus ambako alicheza huko kabla ya kwenda Old Trafford.

Mkataba wa nyota huyo mshindi wa Kombe la Dunia na Ufaransa mwaka 2018, unamalizika Juni mwaka huu.

Pogba amerejea dimbani hivi karibuni baada ya kupona jeraha la kifundo cha mguu na kupiga michezo miwili ya mwisho ya timu yake dhidi ya AC Milan (Ligi ya Europa) na Leicester City (Kombe la FA).

Aidha, ripoti imeeleza kuna uwezekano mkubwa wa Pogba kurudi kwenye timu yake ya Juventus baada ya kumalizika kwa mkataba wake United.

Pogba alianza kuichezea Manchester United mwaka 2011 hadi 2012 halafu akaenda Juventus kati ya mwaka 2012 na 2016 na kurejea tena United mwaka 2016.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND AKARIBIA KUSAJILIWA BARCA

●●● Baba, wakala wa mshambuliaji huyo watua Barcelona kwa ajili ya kufanya mazungumzo...

**BARCELONA,** Hispania

ERLING Haaland huenda akatua katika dimba la Camp Nou baada ya wawakilishi wake kuanza mazungumzo na klabu ya Barcelona, kwa mujibu wa AS.

Alhamisi asubuhi baba wa mshambuliaji huyo ambaye ni mshauri wake, Alf-Inge Haaland na wakala Mino Raiola walionekana katika uwanja wa ndege wa Barcelona.

Kulingana na vyanzo vya habari vya michezo wa nchini Hispania wawili hao walionekana wakiendeshwa kwenye gari na rais wa klabu ya Barcelona, Joan Laporta.

**Rais huyo mpya alimworodhesha straika huyo wa Borussia Dortmund wakati wa kampeni kabla ya kushinda kiti cha urais mwezi uliopita.**

Klabu inapitia kipindi kigumu kiuchumi wakati pia inajaribu kurekebisha mkataba wa mshambuliaji Lionel Messi ambao unatarajiwa kumalizika ifikapo Juni, mwaka huu.

Lakini taarifa zinadai Raiola na Laporta wamekuwa na uhusiano imara wa kufanya kazi pamoja, hivyo basi kuna uwezekano mkubwa wa Barca kushinda mbio za kumnasa Haaland.

Gazeti la The Sun liliripoti wiki hii kwamba, dili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 linaweza kugharimu kiasi cha pauni milioni 300.

Hiyo itajumuisha pauni milioni 150 ya ada ya uhamisho na mkataba wa miaka mitano utahusisha mshahara wa pauni 600,000 kwa wiki.

## ZISIKUPITE

### AGUERO ANUKIA CHELSEA

CHELSEA ipo kwenye nafasi nzuri ya kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Sergio Aguero, 32, atakapoondoka Manchester City mwishoni mwa msimu huu, wakati mchezaji huyo ameweka nia ya kusalia katika Ligi Kuu England. ***(Mail)***

### BENFICA YAMTAKA AGUERO

KLABU ya Benfica ya nchini Ureno nayo inahusishwa na mpango wa kutaka kumsajili, Sergio Aguero, 32, kama akiondoka Manchester City mwisho mwa msimu huu. ***(Record, via Mirror)***

### KLABU ULAYA VITANI

ARSENAL na Independiente, klabu ya nchini Argentina ambako Sergio Aguero alianza kucheza soka la kulipwa, pia zinasemekana kuwa miongoni mwa zinazomkodolea macho ikiwamo Barcelona, Juventus na Paris St-Germain zinazotaka kumsajili msimu huu. ***(Sun)***

### DEPAYE AGOMBEWA

LIVERPOOL huenda "ikapambana" na Barcelona katika kumwania mshambuliaji wa Lyon na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Memphis Depay, 27, ambaye atakuwa huru mwisho wa msimu huu. ***(Marca)***

### LIVERPOOL YAJITOA

KLABU ya Liverpool imejiondoa kwenye mbio za kuwania saini ya mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Norway, Erling Haaland, 20 ***(Football Insider)***

### MESSI AITEGA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi, 33, ametoa orodha ya matakwa yake kwa rais wa Barcelona, Joan Laporta kwa kile anachohitaji ili asaini mkataba mpya hapo Nou Camp. ***(Eurosport)***

### TORREIRA KUTUA BOCA

KIUNGO wa kati wa Arsenal raia wa Uruguay, Lucas Torreira (25), ambaye yuko kwa mkopo Atletico Madrid amesema anataka kurejea Amerika Kusini baada ya kutokea kwa kifo cha mama yake. Na sasa amelenga kujiunga na Boca Juniors ya Argentina ili kutimiza ahadi aliyoweka kwa baba yake. ***(ESPN Argentina, via Goal)***

### GALLAGHER SOKONI

KOCHA wa West Brom, Sam Allardyce anataka kusajili kiungo wa kati, Conor Gallagher ambaye anacheza kwa mkopo kule Chelsea. ***(Metro)***

### LACAZETTE KUJIULIZA

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema hatima ya mshambuliaji wa Ufaransa, Alexandre Lacazette, 29, itajadiliwa mwishoni mwa msimu huu. Nyota huyo amekuwa akihusishwa na AS Roma, Atletico Madrid na Sevilla, huku akiwa amebakiza miezi 12 katika mkataba wake wa sasa. ***(Guardian)***

### REISS ANUKIA OLYMPIAKOS

KLABU ya Olympiakos inafikiria kufanya uhamisho wa mkopo kwa winga wa Arsenal, Reiss Nelson mwenye umri wa miaka 21. ***(Football London)***

HABARI MICHEZO

# NAMUNGO FC YAPANIA USHINDI KUMUENZI JPM

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Namungo FC wamesema wamepania kusaka ushindi katika mechi yao dhidi ya Nkana itakayochezwa kesho ili kumuenzi aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Pombe Magufuli.

**Ofisa Habari na Mawasiliano wa Namungo, Kindamba Namlia, alisema wanafahamu mechi hiyo itakuwa ngumu na yenye ushindani, lakini wamejiandaa kupata matokeo chanya katika kipindi hiki cha maombolezo kwa sababu ya kumuenzi kiongozi huyo aliyefariki Machi 17, mwaka huu hapa jijini Dar es Salaam.**

"Vijana wako sawa kwa ajili ya mchezo. Ni wiki nzima sasa tunajiandaa kwa ajili ya mechi hiyo. Tunaomba Mwenyezi Mungu vijana wawe sawa kiafya hadi siku ya mchezo ili waende kufanya kile ambacho kocha wetu, Hemed Morocco amewaelekeza wafanye," alisema Kindamba.

Kiongozi huyo alisema wageni wao walitarajia kuwasili nchini jana tayari kwa mchezo huo wa hatua ya makundi utakaochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

"Kwanza tunaipongeza sana TFF (Shirikisho la Soka Tanzania), kwa kupambana hadi kufanikisha ruhusa kwa mashabiki kuhudhuria mechi yetu. Lakini pamoja na hayo, ruhusa hiyo imekuja na masharti mengi ambayo moja tu likikiukwa tunaweza kurudi kule kule, kucheza tena bila mashabiki, kwa hiyo inabidi tuwe waangalifu sana, " Kindamba alisema.

Aliongeza uamuzi uliofikiwa umetolewa na maelekezo maalum jinsi ya mashabiki wanavyotakiwa kuingia, kukaa uwanjani na taratibu nyingine, hivyo kwa siku hizi wanachofanya ni kuwapa elimu mashabiki wao jinsi gani ya kufanya.

"Na wamesema watatufutia na hii yote ni kutokana na ugonjwa wa COVID-19 unaoletwa na virusi vya corona na wala si kingine, kwa hiyo tutakuwa waangalifu." Alisema.

Hii itakuwa mechi ya pili kwa Namungo iliyoko kwenye Kundi D ambapo Machi 17, mwaka huu ilichapwa mabao 2-0 na Pyramids ya Misri ikiwa nyumbani huku ilipocheza ugenini ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Raja Casablanca ya Morocco.

Shirikisho la Soka Afrika (CAF), pia limeruhusu mashabiki wasiozidi 10,000 kuingia uwanjani kushuhudia mchezo wa Kundi A wa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya wenyeji Simba dhidi ya AS Vita kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), utakaochezwa leo jijini.




Magolikipa wa Timu ya Soka ya Taifa ya Ufukweni wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya marudiano ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (AFCON- Beach Soccer), dhidi ya Burundi itakayochezwa leo kwenye Ufukwe wa Coco jijini Dar es Salaam. Fainali za michezo hiyo zitachezwa nchini Senegal baadaye mwaka huu. **PICHA: TFF**

## Biashara United yaihofia Polisi TZ

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Biashara United kimeandaa programu maalumu ya mazoezi kwa ajili ya kuhakikisha wanalipa kisasi cha kufungwa na Polisi Tanzania watakapokutana katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Aprili 9, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Karume ulioko Musoma mkoani Mara.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushiriki, Moshi Polisi Tanzania ilipata ushindi wa bao 1-0.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Msaidizi wa Biashara United, Marwa Chamberi, alisema kikosi chake kimeimarika na kila mchezaji amejiandaa kucheza katika kiwango cha juu ili kuondoka na ushindi.

"Wachezaji wote wapo vizuri, kila mmoja ana shauku ya kupata ushindi tukiwa kwenye uwanja wetu wa nyumbani, ingawa tunajua mechi zote za hatua hii ya lala salama ni ngumu," alisema Marwa.

Kocha huyo alisema mara zote wanapokutana na Polisi Tanzania mchezo huwa na ushindani mkubwa hivyo wamelazimika kuongeza mazoezi kwa ajili ya kuhakikisha wanafanya vyema katika mechi hiyo.

Kuhusu ratiba mpya, kocha huyo alisema iko vizuri na wachezaji wake wameahidi kuendeleza kasi ya ushindi na hatimaye kumaliza kwenye nafasi za juu katika msimamo.

## Michuano tenisi yapigwa kalenda

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya tenisi kwa ngazi ya vilabu ambayo yalitarajiwa kufanyika kati ya Aprili 21 na 22, mwaka huu jijini Dar es Salaam yamesogezwa mbele mpaka hapo yatakapotangazwa baadaye, imefahamika.

Kocha wa Klabu ya Gymkhana jijini, Ramadhani Jerani, alisema mashindano hayo yanatarajiwa kushirikisha klabu zote zilizosajiliwa za mchezo huo hapa nchini.

"Wachezaji wangu wanaendelea na mazoezi huku wakisubiri tarehe mpya ya mashindano kutangazwa, tumejipanga kufanya vizuri kwa sababu kila mchezaji anahitaji zawadi siku hiyo," alisema Ramadhani.

Kocha huyo alisema mashindano hayo yatashirikisha vijana wenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea na yana lengo la kuinua vipaji katika mchezo huo.

"Tumeamua kusimamisha mashindano baada ya kutokea msiba mkubwa wa kuondokewa na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Pombe Magufuli, tutajipanga upya maombolezo yakimalizika," kocha huyo alisema.

Aliongeza klabu zote zinatakiwa kuendelea na mazoezi kwa sababu ya kuwa tayari na kuonyesha ushindani wakati ratiba mpya itakapotangazwa.

## *Mrajisi michezo Z'bar atema cheche*

**Na Hawa Abdallah**, ZANZIBAR

MRAJISI wa Vyama vya Michezo Zanzibar, Abubakar Lunda, amevitaka vyama mbalimbali vyote vya michezo Visiwani hapa kufuata katiba zao ikiwamo kufanya uchaguzi pale viongozi waliopo wanapomaliza muda wao wa kukaa madarakani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lunda alisema vyama vingi vimekuwa vikijiendesha kinyume na katiba zao na kuwakumbusha viongozi wake kubadilika.

Lunda alisema licha ya kukabiliwa na ukata, lakini tatizo kubwa la viongozi ni kushindwa kuendesha michakato ya uchaguzi pale wanapofikia mwisho wa uongozi.

"Kutofanya uchaguzi kwa wakati kunawanyima fursa wanachama wao kuchagua viongozi ambao watawaongoza kwa muda kama ambavyo katiba zao zilivyowekwa," alisema Lunda.

Alisema viongozi kuendelea kuvunja katiba za vyama vyao kunachangia kuwapo kwa migogoro na wanachama wao ambayo haisaidii maendeleo ya michezo hapa nchini.

Aliongeza ofisi yake imejipanga kutembelea vyama vyote ili kutoa elimu na kukumbusha umuhimu wa kufuata katiba zao kwa maslahi ya maendeleo ya michezo Zanzibar.

# Michezo

Jumamosi Aprili 3, 2021
Nipashe



Haaland akaribia kusajiliwa Barca UKURASA 22



Nahodha na mshambuliaji wa Simba, John Bocco akizungumzia maandalizi ya mechi Kundi A ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: SSC**

## TFF yampeleka Mwakalebela 'jela'

**Na Saada Akida**

KAMATI ya Maadili ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imemfungia Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela kifungo cha miaka 10 cha kutojishughulisha na mpira wa miguu pamoja na kumtoza faini ya Sh. milioni saba baada ya kutiwa hatiani na makosa mawili ya kimaadili.

Taarifa iliyotolewa na Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, imesema Mwakalebela ametiwa hatiani kwa kosa la kutoa maneno ya uchochezi kwa nia ya kuchochea mashabiki na wanachama wa Yanga dhidi ya vyombo vinavyosimamia mpira wa miguu nchini.

Ndimbo alisema kwa kosa hilo Mwakalebela amefungiwa miaka mitano na faini ya Sh. milioni tano na uamuzi huo wa Kamati umetolewa kwa kuzingatia kifungu cha 73 (4), cha Kanuni za Maadili za TFF toleo la mwaka 2013.

Ofisa huyo alisema Mwakalebela alilalamikiwa kwa kuitisha mkutano na waandishi wa habari uliofanyika Februari 19, mwaka huu kwa kudai TFF, Bodi ya Ligi (TPLB) na Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi zinaihujumu Yanga, madai ambayo alishindwa kuthibitisha mbele ya kamati.

"Shtaka la pili alilalamikiwa kwa kutoa taarifa za uongo, Oktoba Mosi, 2020 aliitisha mkutano na kudai kuwa anao mkataba kati ya Bernard Morrison na klabu ya Simba na kuonyesha kwa waandishi wa habari huku akijua ni uongo na kinyume cha sheria," alisema Ndimbo.

Alisema kupitia shtaka hilo, kamati imempa onyo la kutenda kosa hilo kwa muda wa miaka mitano pamoja na kumtoza faini ya Sh. milioni mbili na adhabu hizo zimetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 6(1) b na 6(1)c cha Kanuni za Maadili za TFF toleo la 2013.

Ndimbo alisema Mwakalebela anaruhusiwa kukata rufani kwenye kamati husika endapo hataridhika na uamuzi wa kamati hiyo ya maadili. Baada ya adhabu hiyo kutangazwa jana jijini, Mwakalebea alisema kwa kifupi: 'Yote maisha."

# Simba, AS Vita hatumwi mtoto

**Na Saada Akida**

## ●●● Mnyama ahitaji pointi moja kutinga hatua ya robo fainali, Bocco atoa neno...

KATIKA kuhakikisha inatinga mapema hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kikosi cha Simba kinashuka kuwakabili AS Vita kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) katika mechi ya Kundi A itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ikiwa na kauli mbiu ya 'DO or DIE SEASON TWO.'

**Simba ndio vinara wa Kundi A wakiwa na pointi 10 wakifuatiwa na Al Ahly yenye pointi saba, AS Vita yenye pointi nne huku mabingwa wa Sudan, Al Merreikh wenye pointi moja mkononi wakiburuza mkia.**

Wawakilishi hao wa Tanzania wanahitaji pointi moja tu ili watinge hatua ya robo fainali kabla ya kusafiri kwenda Cairo, Misri kuwavaa wenyeji Al Ahly katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Simba inashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kupata ushindi mara mbili dhidi ya AS Vita, baada ya misimu miwili iliyopita kuwafunga mabao 2-1 hapa nyumbani na msimu huu walipokutana katika mchezo wa kwanza ugenini Kinshasa kushinda bao 1-0.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Seleman Matola, alisema wamejiandaa vizuri kwa ajili ya kutafuta ushindi katika mchezo huo muhimu ili kujihakikishia kucheza robo fainali ya michuano hiyo.

Matola alisema kikosi chao kipo vizuri na hakuna mchezaji ambaye watamkosa huku wakiwa wamejipanga kucheza kwa nidhamu ya hali ya juu kwa ajili ya kupambana kutafuta matokeo chanya.

"Tumejiandaa vizuri na kila kitu kinaenda sawa, hakuna majeruhi, kazi iliyobaki ni wachezaji kwenda kufanya majukumu yao ya uwanjani kwa kupambana kutafuta matokeo chanya ili kupata pointi muhimu zitakazotuhakikishia kucheza robo fainali," alisema Matola.

Naye nahodha wa Simba, John Bocco alisema wamejipanga vizuri kiakili na kimwili kwa ajili ya mchezo huo huku wakijiandaa kupambana kutafuta matokeo mazuri. Bocco alisema wanahitaji kufikia malengo yao ya kuvuka hatua hiyo ambayo imekuwa mikakati yao mikubwa kwa sasa.

"Tutaingia uwanjani kwa nidhamu ya hali ya juu kwa sababu hatutaingia uwanjani kwa kuangalia historia ya nyuma ya kuwa tumeshinda msimu uliopita nyumbani na mchezo wa kwanza tulishinda kwao,".

"Hatuingii uwanjani kwa dhana hiyo bali tunaenda kupambana kutafuta matokeo mazuri, hautakuwa mchezo rahisi sana kwa pande zote mbili, kwetu na AS Vita," alisema Bocco.

Naye Kocha Mkuu wa AS Vita, Florent Ibenge, alisema ana imani soka lina matokeo matatu ikiwamo kushinda, kupoteza na sare na kwao lakini wao wamekuja kucheza mpira na kuhitaji kupata matokeo mazuri.

"Tumejipanga kufanya vizuri na wachezaji wote tegemeo watacheza akiwamo Shaaban Djumaa, hatuna hofu ila tutacheza kwa nidhamu ya hali ya juu kwa sababu Simba hii ni tofauti na ya msimu uliopita," alisema Ibenge.

Mechi nyingine ya kundi hilo itachezwa jijini Khartoum nchini Sudan kati ya wenyeji Al Merrikh dhidi ya Al Ahly.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >